SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Wakazi** ataka mjadala kukatwa asilimia 30

UKURASA 20



**Harmonize** apeleka joto 'Arizona'

UKURASA 20

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Septemba 19, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya
ISSN 0856 • No. 0580708
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Vigogo kitanzini

• **Ni** walioshindwa kutekeleza agizo la Rais Samia kwa muda mrefu, CCM yatoa siku 30... *Endelea ukurasa 5*



Mwonekano wa daraja jipya la Tanzanite lenye urefu wa km. 1.03 na upana wa mita 20.5, linalounganisha maeneo ya Aga Khan Upanga Mashariki na Oysterbay kupitia Bahari ya Hindi, jijini Dar es Salaam jana. Ujenzi wake umefikia asilimia 93 na linatarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu. **PICHA: WUU**

## Wasomi wamlilia Profesa Luhanga

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

## Nyuma ya pazia mimba shuleni

• **Anayeishi** na bibi afunguka siri nzito, 139 mkoa mmoja, mwaka mmoja... *Endelea ukurasa 4*

MICHEZO YANGA YAMALIZA 'HESABU' NIGERIA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# DMO, mhandisi wasimamishwa madai ubadhirifu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amewasimamisha kazi, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Dk. Janeth Makoye, na Mhandisi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Erick Rugeiyamu, ili kupisha tuhuma zinazowakabili za matumizi mabaya ya fedha za miradi ya afya.

Wakati akichukua hatua hiyo, Mgumba ameagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenda kufanya ukaguzi maalumu katika halmashauri hiyo katika miradi ya afya.

Sambamba na CAG, ametoa siku saba kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Songwe kumpatia taarifa ya uchunguzi juu ya matumizi mabaya ya fedha katika halmashauri hiyo.

Mgumba alichukua hatua hiyo jana, baada ya kukagua ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Igoye, wilayani humo na kubaini kwamba licha ya serikali kupeleka Sh. milioni 50, kazi hiyo haijakamilika.

"Yaani leo (jana) nilipokuja hapa nilifikiri nitakuta madaktari na manesi wapo na wananchi mnapata huduma. Lakini baada ya kukagua jengo humo ndani, sitaki kuwa mnafiki sijafurahishwa.

"Sijafurahishwa kwa kuwa mradi haujakamilika kwa wakati. Nilipowauliza wataalamu wetu wameniambia sababu ni mvua barabara mbaya. Lakini tangu nifike hapa Songwe mwezi wa tano (Mei, mwaka huu) hakuna siku hata moja mvua imenyesha," alisema.

Alisema ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Igoye, ni miongoni mwa miradi ya afya katika halmashauri hiyo ambayo imekuwa na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mgumba alisema katika hali isiyo ya kawaida licha ya serikali kutoa Sh. milioni 50 na wananchi kujitolea nguvu kazi yenye thamani ya Sh. milioni 19, bado ujenzi haujakamilika.

"Haiwezekani wananchi wajenge hadi kuezeka kwa kutumia Sh. milioni 19 halafu serikali ikaunga mkono kwa kutoa Sh. milioni 50 halafu mnaniambia mmeshindwa kukamilisha ujenzi? Hapa kuna matumizi mabaya, hivyo naagiza ndani ya siku saba TAKUKURU mnipatie taarifa," alisema.

"Halafu unaambiwa fremu ya mlango ule pale imenunuliwa kwa gharama ya Sh. 230,000 haiwezekani. Hapa viongozi wamehusika kupotosha, Mkurugenzi upo hapa nakuagiza wasimamishe kazi DMO (Mganga Mkuu) na mhandisi halafu na TAKUKURU nawapa siku saba mnipatie taarifa na anzeni na hawa.

"Na kwa mamlaka niliyopewa, ofisi yangu pia itaunda kamati maalum ya uchunguzi ili ikifikia wakati wa kuchukua uamuzi tusimuonee wala kumpendelea mtu," alisisitiza RC Mgumba.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Zahanati hiyo, Ephes Kibona, alilalamikia kutishiwa maisha na baadhi ya watendaji wa halmashauri kutokana na msimamo wake wa kutaka taratibu zifuatwe kwenye ununuzi.

# Wasomi wamlilia Profesa Luhanga

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI na wasomi wametuma salamu za rambirambi kufuatia kifo cha aliyewahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Matthew Luhanga, aliyefariki dunia Jumatano.

Prof. Luhanga, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe, alifariki dunia mkoani Dar es Salaam wakati akiendelea na matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimsumbua.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo alisema Profesa Luhanga alikuwa profesa mahiri katika eneo lake na wakati akiwa Rais wa Chama cha Wanafunzi wa UDSM, yeye alikuwa Makamu Mkuu wa chuo hicho na aliwalea vizuri.

"Alitulea na kutuelekeza na ni mtu ambaye alikuwa anavumilia sana, aliruhusu mijadala, aliwaruhusu vijana kubishana naye bila changamoto yoyote na mwisho wa siku aliwaelekeza," Prof. Mkumbo alisema.

Waziri wa zamani, Prof. Mark Mwandosya, akimzungumzia Prof. Luhanga, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, akisema: "Jua limezama leo jioni. Profesa Matthew Laban Pimpa Luhanga, ndugu na rafiki wa karibu, mwanafunzi mwenzangu, profesa mwenzangu, mhandisi mwenzangu, mwandishi mwenza, jirani yangu, ametutoka. Hatunaye tena. Mwenyezi Mungu amrehemu (RIP)."

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. William Anangisye, katika salamu zake za rambirambi, alisema wamepokea kwa masikitiko kifo cha Prof. Luhanga.

Prof. Anangisye alibainisha kuwa Prof. Luhanga alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo hicho kuanzia mwaka 1991 hadi mwaka 2006.

**RATIBA YA MAZISHI**

Msemaji wa Familia, Nehemiah Mchechu, aliyekuwa Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba Tanzania (NHC), alisema jana kuwa maziko ya Prof. Luhanga yanatarajiwa kufanyika Jumanne katika makaburi ya Kwa Kondo, Tegeta mkoani Dar es Salaam.

"Jumatatu (kesho) kuanzia saa nne asubuhi Jumuiya wa Chuo Kikuu itapata wasaa wa kuaga mwili shughuli ambayo itafanyika Ukumbi wa Nkrumah, (ratiba) ambayo itakwenda sambamba na misa maalum itakayofanyika katika kanisa la Chuo Kikuu (Charplain) na baadaye jioni kuanzia saa 12 ibada ya faraja itafanyika nyumbani kwa marehemu," alisema.

Mchechu alisema kuwa Jumanne kuanzia saa 6:30 mchana misa pamoja na shughuli za kutoa heshima za mwisho itafanyika katika Parokia ya Mt. Andrea Mtume, Bahari Beach na kuanzia saa 10 jioni msafara utaelekea mkaburini kwa ajili ya maziko.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuondoka kuelekea New York nchini Marekani kuhudhuria Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. **PICHA: IKULU**

# Vyama 16 vyachukua fomu uchaguzi mdogo wa Ushetu

**Na Waandishi Wetu**

VYAMA 16 vya siasa vimejitokeza kuchukua fomu za uteuzi kugombea kiti cha ubunge katika Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Ushetu, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Mkoa wa Shinyanga unaotarajiwa kufanyika Oktoba 9, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), vyama vilivyojitokeza kuchukua fomu za uteuzi hadi kufikia jana saa 10:00 jioni ni pamoja na DP, CHAUMMA, NRA, ADC, AAFP, Sauti ya Umma (SAU).

Vingine ni ADA TADEA, UPDP, TLP, Demokrasia Makini, UMD, NLD, UDP, CCK, CCM na ACT-Wazalendo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, tume hiyo ilibainisha kuwa imeshuhudia baadhi ya wagombea wakichukua fomu za uteuzi huku kikuwapo na ushindani kati ya wanawake na wanaume ambapo kati ya vyama 16 vilivyochukua fomu, vyama vinane vimewakilishwa na wanawake.

Vyama vilivyoteua wawakilishi wanawake kuchukua fomu za uteuzi ni ADC, AAFP, SAU, ADA-TADEA, UPDP, UMD, NLD na CCK.

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ushetu, Linno Mwageni, alisema fomu za uteuzi kwa wagombea wa kiti cha ubunge wa jimbo hilo zilianza kutolewa Septemba 13 na uchukuaji wa fomu hizo unatarajiwa kufikia ukomo leo ambayo pia itakuwa nu siku ya uteuzi wa wagombea.

Msimamizi Msaidizi wa Jimbo la Ushetu, Godfrey Lwambura, aliwataka wagombea hao kuhakikisha wanajaza fumo za uteuzi kwa usahihi na siku watakaporejesha fomu hizo watajaza Fomu Namba 10 ya kuheshimu maadili ya uchaguzi.

Kwa mujibu wa ratiba ya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Ushetu iliyotolewa na NEC, kampeni za uchaguzi zitaanza kesho hadi Oktoba 8, mwaka huu na siku ya kupiga kura itakuwa Oktoba 9, mwaka 2021.

**■Imeandikwa na Felister William, Edwin Mosha na Irene Mwakatobe (TUDARCo)**

## HABARI KITAIFA

# Corona yakwamisha mamia mafunzo India

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema mlipuko wa corona umesababisha wanufaika 721 wa Mpango wa Mafunzo Ushirikiano wa Kiufundi na Kiuchumi wa Serikali ya India (ITEC) kushindwa kwenda kwa ajili ya mafunzo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo juzi jioni wakati Tanzania na India zikisherehekea ushirikiano huo ambao ulianza mwaka 1972 na kuwezesha Watanzania kwenda India kupata mafunzo mbalimbali.

Prof. Ndalichako alisema katika mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20 jumla ya nafasi 721 zilitolewa lakini kutokana na mlipuko wa corona, wengi wao hawakwenda mafunzoni.

"Wanufaika ni watumishi katika taasisi za kawaida na pia hutoa nafasi kwa majeshi yetu kushiriki pamoja na watu wanaohusika na masuala ya sheria, wapo Watanzania wengi wanaofanya mafunzo haya India ambao ni takribani 3, 000," alisema.

Waziri huyo aliongeza kuwa Serikali ya India imekuwa ikiisaidia Tanzania katika kuhakikisha nchi hizo zinafurahia uhusiano mkubwa ambao ulianzishwa na waasisi wa mataifa hayo.

"Tanzania kupitia programu ya ushirikiano katika masuala ya teknolojia na uchumi tumepeleka wanafunzi wengi India kusoma, tulianza mwaka 1972 na wanafunzi 24 na idadi imekuwa ikiongezeka hadi kufikia mwaka 2017/18 jumla ya nafasi 474 zilitolewa kwa Tanzania," alisema.

Waziri huyo alisema nchi hizo zimekuwa zikishirikiana katika masuala mengi kwa kuhakikisha wanajenga nguvu kazi wenye weledi uliosheheni ujuzi na maarifa unaohitajika katika dunia ya sasa.

Pia alisema nchi hizo zimekuwa zikishirikiana katika masuala ya teknolojia katika uanzishaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

Alisema kupitia ushirikiano kati ya nchi hizo, wameanzisha mafunzo ya hali ya juu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Taasisi ya Nelson Mandela, Arusha na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam ambapo India imewezesha upatikanaji wa vifaa vya kisasa zikiwamo kompyuta.

Pia alisema wamepeleka walimu India kusoma ili kuimarisha ujuzi na maarifa katika fani za TEHAMA na wapo ambao wamepata mafunzo katika ngazi ya Stashahada ya Juu (Post Graduate Diploma).

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, alisema kila mwaka wamekuwa wakisherehekea uhusiano huo ambao unawaleta pamoja wanufaika na kueleza uzoefu wao waliopata India.

Alisema programu ya ITEC ilianza Septemba 15, 1964 na imekuwa muhimu kwa nchi yao kutoa msaada wa kiufundi, uhamishaji wa teknolojia na kujenga uwezo kwa nchi washirika.

"Kwa Tanzania programu hii ilianza mwaka 1972, ilianza na wanufaika 24 na kila mwaka wameongezeka hadi nafasi 500. Zaidi ya raia 4,500 wakiwamo maofisa wapatao 300 wa jeshi nao wananufaika na mpango huu," alisema.

Mnufaika wa programu hiyo, Elibahati Kimaro kutoka Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, alisema alikwenda India mwaka 2019 kusoma masuala ya taka ngumu za mijini na baada ya kurudi ameanzisha uzalishaji wa mbolea kwa kutumia mabaki mbalimbali ya shambani.



Wakurugenzi wa Halmashauri za Magu, Nzega, Mkalama na Kondoa pamoja na wanasheria wao wakionyesha hati za makubaliano kati ya Halmashauri zao na Wakala wa Maji safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuhusu uchimbaji wa visima, mabwawa madogo, malambo na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji maji ya mvua, baada ya kutiliana saini katika Ofisi ya Makamu wa Rais, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Majaliwa aonya rushwa watumishi

**Na Mwandishi Wetu,**
KIBONDO

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa (pichani), amewataka watumishi wa umma kufanya kazi kwa weledi, uaminifu na uadilifu ili kuleta matokeo chanya, huku akiwataka kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Vilevile amewataka watumishi hao wahakikishe wanafanya kazi ya kutoa huduma kwa wananchi kwa kufuata taratibu zilizowekwa pamoja na kusimamia vizuri fedha za miradi ya maendeleo zinazopelekwa katika maeneo yao.

Alielekeza hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa umma wilayani Kibondo akiwa katika ziara ya kikazi kukagua



miradi ya maendeleo na shughuli za kijamii mkoani Kigoma.

Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan anatarajia kuona mipango yote ya serikali inatekelezwa katika jamii kwa kufanya kazi kwa bidii.

"Wito wa Rais Samia ni kuona uchumi unaenda kwa kasi kuanzia mtu mmoja mmoja, jamii na taifa kwa ujumla, tulianza na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili kuwawezesha Watanzania kufanya shughuli zao za kiuchumi," alisema.

Waziri Mkuu aliwataka watumishi hao kuwahamasisha na kuwawezesha Watanzania kujishughulisha katika shughuli za kiuchumi.

"Kama ni mkulima alime sana, kwenye migodi wafanye kazi sana, wafanyabiashara wafanye sana biashara hata wanaosoma wasome sana," alisisitiza.

Waziri Mkuu alisema watumishi wanapaswa washiriki kikamilifu katika kusimamia makusanyo ili kuwawezesha kutekeleza miradi wanayoiona italeta tija kwa wananchi.

"Kigezo cha ukusanyaji wa mapato kipimwe kutokana na ujenzi wa miradi ambayo inawahudumia wananchi," alisema.

Waziri Mkuu pia aliwaagiza wakuu wa wilaya wahakikishe miradi yote inayotekelezwa inakuwa na thamani ya fedha iliyotolewa.

"Wakurugenzi simamieni utekelezaji wa miradi katika maeneo yenu ili wakuu wa wilaya wakija kuizindua, ionekane thamani ya mradi huo," Majaliwa aliagiza.

# Serikali yapata dawa matatizo sugu ushirika

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema kumekuwa na mitazamo tofauti miongoni mwa wadau kuhusu sababu ya kuwapo kwa matatizo sugu ya ushirika na namna ya kushughulikia.

Wadau wengi wa ushirika nchini wamekuwa na mtazamo kwamba matatizo sugu ya ushirika nchini yanatokana na sababu mbalimbali na miongoni mwake ni upungufu wa sheria inayosimamia sekta ya ushirika nchini, Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema jana mkoani Dar ers Salaam kuwa kwa sasa serikali imekuja na mwarobaini wa kutatua matatizo hayo.

Prof. Mkenda alikuwa anafungua kikao cha wadau wazoefu wa ushirika kujadili mapendekezo na marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013.

Waziri Mkenda alisema kufuatia mtazamo wa wadau na dhamira ya kutatua matatizo sugu ya ushirika yanayotokana na upungufu wa sheria, mwaka 2019 serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilielekeza Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuanza mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria ya Vyama Vya Ushirika.

Katika mkutano huo, Waziri Mkenda alimpongeza Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, kwa kufanikiwa kuwaalika wadau wote wazoefu katika kikao hicho kwa ajili ya kutoa maoni.

Vilevile, Waziri Mkenda ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na Wizara ya Kilimo kuhakikisha maoni yatakayotolewa na wadau katika kikao hicho yanazingatiwa katika mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika unaoendelea.

RIPOTI MAALUM

# Nyuma ya pazia mimba shuleni

**Na Elizabeth Zaya**

## ■Anayeishi na bibi afunguka siri zote
## ■139 wapata ujauzito mwaka mmoja



MIAKA inapita, kimedumu kuwa kitendawili endelevu kisicho na majibu kwa waliokishikilia Kiswahili kwamba mimba hazikomi kwa mabinti wadogo wanaostahili kuwa darasani na hata kanuni za afya hazikubaliani kwa umri wao kubeba ujauzito.

Ushuhuda upo wazi, juhudi za kidola na kijamii zimepita, lakini mavuno ya kuhesabu. Mamlaka nazo zashika kichwa "kulikoni?"

Hapo ndipo Nipashe Jumapili inapojipa wajibu kujitosa kupekua kinachojiri kwa majirani wa ofisi zake Mkoa wa Pwani ambako rekodi ya mimba kwa mabinti hazitamanishi.

Baada kupata faragha, vikubwa kati ya mengi ni makuu matatu; utamaduni, elimu duni na umaskini, vyote vikiikamata jamii na kusababisha madhila kwa mabinti.

Ni butwaa lililomwangukia mwandishi pale binti anyehitaji ulinzi na malezi ya mzazi, anaishi na bibi anayemlea kwa staili ya 'mtu na shoga yake', pia ni mwanafunzi mwenye jukumu kuu la kuwa mwenyeji wa huduma ya vilevi kwa watu wazima, baadhi yao ni 'fisi wa ngono'.

Gazeti hili linaamua kuzama kwa wahusika kufukua mzizi wa tatizo. Fuatilia:

"Huwa ninafanya biashara hii ya kuuza pombe ili tuishi mimi na bibi yangu," ni sauti ya Chausiku (sio jina lake halisi), binti wa miaka (13), mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Kerege, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, anayesimulia hali ya maisha anayoishi.

Majira ya saa nne asubuhi, akiwa anafungasha pombe kwenye makopo, Chausiku (14) anaendelea kuwasilisha akiwa katika hali ya utulivu na sauti ya chini, akisema:

"Inanibidi nitumie akili nyingi kupanga ratiba yangu ya shule vizuri ili majukumu ya nyumbani na shuleni niyatimize na wakati mwingine nikizidiwa hunibidi niweke shule pembeni kidogo, nitafute hela ya chakula kwanza.

"Wazazi wangu walifariki dunia nikiwa mdogo sana, kwa hiyo nilibaki hapa kulelewa na bibi yangu. Kabla bibi hajazeeka sana maisha yetu hapa yalikuwa na ahueni kidogo, kipindi hicho alikuwa na nguvu ya kufanya vibarua.

"Maisha yalianza kuwa magumu tangu nilipoingia darasa la saba, zile kazi ambazo bibi alikuwa akizifanya ili tupate chakula, sasa hazifanyi tena, hana nguvu tena. Sasa anatengeneza pombe na kuweka kwenye hivi viroba vya Sh. 350 na 500 na kunipatia nikauze ili tupate pesa ya kujikimu.

"Nilianza kuuza pombe hizo kwa kutembeza mtaani miaka mitatu iliyopita, mpaka sasa ninaendelea kama unavyoona hapa ninaandaa, nina wateja wangu maalum, vituo vyangu vya kupeleka huwa ninavifahamu kabisa.

"Ninafanya hivyo siyo kwa kupenda, bali kutokana na hali ya umaskini inayotukabili mimi na bibi yangu na nisipofanya hivyo hatuwezi kupata pesa ya kula na mahitaji yangu shuleni.

"Nilipochaguliwa kuingia sekondari, kidato cha kwanza, hali ilizidi kuwa mbaya zaidi kwa sababu ratiba za shuleni zilianza kunibana lakini nilikuwa ninalazimika wakati mwingine kuacha kwenda shuleni au kutoroka baadhi ya vipindi ili nikauze pombe kwa sababu nisipofanya hivyo tunalala njaa.

Binti huyo anasema kwa siku ambazo haendi shuleni, huwa anaomba madaftari kwa wanafunzi wenzake na kunakili walichokiandika kisha kujisomea akiwa nyumbani, akikabiliwa na kikwazo kingine cha kuishi kwenye nyumba isiyokuwa na huduma ya umeme.

"Na mpaka hapa nimefika kidato cha tatu ni nguvu za Mwenyezi Mungu, lakini bado sijakata tamaa, ninauza pombe ili nipate fedha kujikimu kimaisha na bibi yangu, ninaamini Mungu atanisaidia na nitafaulu kuingia kidato cha tano na nitafaulu kwenda chuo kikuu," anasema.

Chausiku anabainisha kikwazo kikuu katika biashara yake hiyo ni asilimia kubwa ya wateja wake kuwa wanaume, wengi wao wakimtaka kimapenzi na wengine kumshawishi aache biashara hiyo ili wamuoe.

"Ninakutana na vishawishi vingi kwa kweli, tena wanaume wengine ni watu wazima, wakiniona tu kwa sababu wanafahamu kwamba mimi huwa ninauza pombe, wananiita. Wananunua lakini wanakuwa wanitongoza, ninakutana na mambo mengi lakini huwa ninakataa," anabainisha.

**ANGALIZO LA BIBI**

Nuru Hashim, bibi wa chausiku, anasema alianza kumlea binti huyo akiwa na umri mdogo baada ya wazazi wake kufariki dunia.

"Kipindi hicho mahitaji ya kawaida ikiwamo kumpatia chakula hayakuwa shida kubwa sana, sasa sina nguvu na ninaugua, siwezi kufanya kazi ngumu ndio maana inabidi afanye yeye ili tupate pesa ya kula.

"Nilimfundisha kuandaa hiyo pombe kwa sababu sikuwa na namna nyingine ya kufanya kwa sababu hata wale waliokuwa wanatusaidia tunapokosa chakula baada ya mimi kuanza kuugua, walipunguza ukaribu na sisi, wakati mwingine tunakosa chakula ndani.

"Jambo kubwa ambalo huwa ninamwambia ni kuwa mwangalifu na wanaume wadanganyifu huko anakouza pombe, asikubali kudanganyika au kuingia tamaa kwa sababu wanaume wengi ni waongo," Nuru anaonya.

Katika majumuisho ya simulizi ya maisha ya familia hiyo, Nipashe Jumapili ilibaini kipato duni katika familia, ni sehemu ya mzizi wa mabinti wengi mkoani Pwani kukatisha masomo yao, ingawa kuna madhila mengine ukiwamo utamaduni wa jamii hiyo.

Mwalimu Mlezi wa Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kerege, Sophia Mohamed, anasema tangu awe mlezi wa wanafunzi shuleni huko, amekuwa wakikumbana na shida mbalimbali za wanafunzi, nyingi zikiangukia kuhitaji msaada wa kibinadamu.

Mwalimu Sophia pia anakiri kumfahamu mwanafunzi anayeuza pombe ili kumlea bibi yake, akisema: "Nilipogundua kwamba anaishi kwenye mazingira magumu, nilizungumza naye kwa kina na nikagundua hafanyi biashara hiyo kwa kupenda.

"Baada ya kufahamu shida anazopitia, sikuwa na namna ya kufanya zaidi ya kumshauri na kumweka karibu na mimi ili asijione mnyonge na asichukue uamuzi ambao unaweza kumharibia kabisa maisha yake ya baadaye.

"Nilimshauri ajipangie ratiba yake vizuri na ahakikishe hakosi shuleni na akazane kwenye masomo kwa sababu ndiyo yatakuwa mkombozi kwake, nilizungumza kama mzazi ikiwezekana kutafuta kitu kingine ambacho atakifanya baada ya masomo na aachane na kuuza pombe.

"Na kila mara ninakuwa ninamwita, ninazungumza naye kama mtoto, ninaamini kwamba itafika wakati atakuwa sawa na ataacha hii biashara na mimi pia ninamsaidia pale ninapopata chochote."

Mwalimu Sophia anabainisha kuwa shuleni anakofanyia kazi kuna kesi nyingi za watoto kuishi na bibi na hali duni ya maisha kwa wanafunzi.

**UHUSIANO WA KIMAPENZI**

Mwalimu huyo anabainisha kuwa kuna tatizo kubwa la watoto kuacha shule kutokanana na hali ngumu kimaisha kwenye familia wanazotoka.

Vilevile, anasema wapo baadhi yao ambao huamua kujiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi wao kwa wao ili kusaidiana na kuna kundi la pili la wanaoamua kujiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi na watu wazima ili kutimiziwa mahitaji yao, vyote vikiangukia kwenye mimba za utotoni na madhila mengine kiafya.

"Kuna kipindi nilibaini kwamba kuna baadhi ya wanafunzi wanajihusisha kwenye uhusiano wa kimapenzi wenyewe kwa wenyewe hapahapa shuleni ili kupata msaada wa chakula au nauli kutoka kwa wenzao ambao wazazi wao wana uwezo wa kuwapatia pesa ya kutosha.

"Nilibaini hilo baada ya kuona kuna watoto ambao ninawafahamu walikuwa na maendeleo mazuri sana shuleni na walikuwa wanafaulu vizuri sana, lakini ghafla wakaanza kushuka, ilibidi niwaite ofisini lakini walikuwa hawataki kueleza vizuri, walikuwa wanakwepakwepa hivi.

"Kwa sababu mimi ni mzazi, niliona kama kuna kitu wanaficha na labda wanaogopa kusema, ilinibidi nihamishie ofisi yangu niwe ninakaa nje ya ofisi ya walimu, nikajitenga na kuanza kukaa nje, baada ya kufanya hivyo nilianza kuwaita mmoja baada ya mwingine na kuzungumza nao kirafiki, watoto walianza kunieleza mambo mengi.

"Baadhi yao walisema wanajiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wenzao kwa sababu wanawapatia nauli na chakula hasa hivi vidogo vidogo vinavyokuwa vikiuzwa hapa kama mihogo na vinginevyo vya namna hiyo.

"Mwingine anakuambia kwamba anachoka kutembea kila siku kwa miguu kuja shuleni na kurudi kwa kukosa nauli, hiyyo anafikia uamuzi huo ili kupunguza makali ya kutembea kila siku.

"Anakuambia 'madam ninatembea kila siku kutoka Kiharaka hadi Kerege, umbali mrefu kwenda na kurudi kila siku'. Nilipambana sana katika hili kuwakemea na kuwatishia kuwaita wazazi wao, ninaona kwa sasa wanaanza kukaa sawa.

"Lakini kuna shida nyingine kubwa hali ya maisha ya huku ni ngumu. Wakati mwingine ninalazimika kuingia gharama ya kuwanunulia wanafunzi nguo za ndani, ninafikiri unaelewa ninapozungumzia hali ya maisha ya huku, baadhi ya wazazi huwa hawajali watoto wao.

"Wapo baadhi ya wanafunzi wa kike na hata wa kiume ambao hata nguo ya ndani wanakuwa hawana, kwa hiyo ukimwangalia mtoto unaona hayuko sawa na wanakuwa wanyonge, wa kike siku moja niliwakagua, ilikuwa ni aibu.

"Ilinibidi niende Kariakoo kuwatafutia nguo za ndani, hata wa kiume niliwanunulia. Hilo limewafanya sasa waniozee hasa, wananiona kama mama yao. Kuna changamoto kubwa huwa wanakumbana nazo na wakiitwa kwenda kueleza kwenye ofisi ya walimu, wanaogopa, lakini kwangu wananieleza.

"Kuna watoto pia hapa mwaka juzi walikutwa na ujauzito, waliondoka wakiwa wanalia sana, nilizungumza nao na shida kubwa iliyochangia ni sababu hizo hizo za hali duni za kimaisha wanakotoka, watoto wengi wanajilea wenyewe na wengine hao hao ndio wakuu wa kaya, wao ndio wanahudumia familia, kwa hiyo wanajikuta wameingia kwenye vishawishi," anasema.

Mwalimu Sophia ananyoshea kidole kuvunjika kwa ndoa na wazazi kutawanyika kuwa ni sehemu ya mzizi wa mimba za utotoni zinazowakumba mabinti mkoani Pwani.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, mwaka jana pekee, wanafunzi 139 walipata ujauzito na kulazimika kukatisha masomo yao. Kati yao, wa shule za msingi walikuwa 39 na wa sekondari 100.

■ITAENDELEA JUMAPILI IJAYO

HABARI KITAIFA

# Anusurika kifo mgogoro wa makundi ya wafugaji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UMEIBUKA mgogoro baina ya makundi ya wafugaji wa jamii ya Wasukuma na Wamasai huku mmoja wa wafugaji, mkazi wa Kijiji cha Kivungu, Kata ya Kilangali wilayani Kilosa mkoani Morogoro, akinusulika kifo baada ya kukatwa mapanga katika sehemu mbalimbali za mwili wake.

Mfugaji huyo alifahamika kwa jina la Baraka Kisewe, maarufu Mafuriko, ambaye kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya St. Joseph iliyoko Dumila, alidai alifika katika kijiji hicho na ghafla alikutana na kundi hilo la wafugaji jamii ya Wasukuma na kuanza kumshambulia kwa mikuki na sime na kumjeruhi.

"Mimi nilikuwa ninaenda dukani kufuata mahitaji lakini kabla sijafika lilitokea kundi la wafugaji jamii ya Wasukuma na kuanza kunishambulia na mikuki na sime na kunijeruhi, wala sijui chanzo cha kunifanyia unyama huo. Ninaomba serikali iwachukulie hatua wote waliohusika," alisema.

Alisimulia kuwa kutokana na wafugaji hao kuwa wengi, hakuwa na cha kufanya na kulazimika kutii vile alivyokuwa wakitaka baada ya kumshambulia na vitu hivyo vyenye ncha kali na alipopoteza fahamu, walimwacha kwenye eneo hilo.

Muuguzi wa Hospitali hiyo, Ally Mbonye, alithibitisha kumpokea mgonjwa huyo akieleza alikuwa na majeraha yaliyotokana na kuchomwa na vitu vyenye ncha kali na kwa sasa bado anaendelea kupatiwa matibabu.

Leshimile Mlongwa, Makamu wa Raigwanani Kanda ya Ngaite wilayani Kilosa, alisema vijana wa jamii ya wafugaji waliofanya vitendo hivyo wanafahamika lakini mpaka sasa hawajachukuliwa hatua zozote wakati suala hilo limeripotiwa polisi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, Majid Mwanga, alikiri kutokea kwa tukilo la kushambuliwa kwa mfugaji huo na tayari ameshaliagiza Jeshi la Polisi wilayani humo kuwatafuta watuhumiwa hao.

Alibainisha kuwa tayari ameshawakutanisha viongozi wa pande mbili za wafugaji hao ili kuwasisitizia juu ya umuhimu wa kuishi kwa amani kwa kufuata sheria za nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela, alionya makundi ya wafugaji kuacha mara moja kuanzisha migogoro ya wao kwa wao pamoja na makundi ya wakulima kwa kulishia mifugo katika mashamba ya wakulima, akisisitiza serikali itawachukulia hatua kali wote watakaobainika kuanzisha migogoro hiyo.

# Vigogo kitanzini agizo la Samia

**Na Beatrice Shayo,** MTWARA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetoa mwezi mmoja kwa viongozi wa serikali kutatua mgogoro wa wananchi wanaodaiwa kuvamia katika eneo la uwanja wa ndege mkoani Mtwara.

Agizo hilo lilitolewa jana mkoani hapa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, alipofanya ziara kwenye uwanja mpya wa ndege Mtwara na kuzungumza na abiria walioshuka ikiwa ni mara ya kwanza kutua kwa ndege katika uwanja huo.

Alisema mgogoro huo ni wa siku nyingi na tayari Rais Samia Suluhu Hassan alishatoa maelekezo kwa wahusika kutatua mgogoro huo lakini hadi sasa tatizo halijatatuliwa.

Shaka alisema masuala ya msingi ambayo yanawagusa wananchi wakati umefika wa kuyatatua kwa wakati badala ya kuisababishia serikali hasara.

"Tunapokuwa na changamoto kama hizi ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja, kipaumbele cha kwanza kwa serikali ni kuona namna gani ya kutatua kwa wakati, kama mngeutatua hili tatizo ina maana hata mimi nisingekuta huu mgogoro," alisema.

Shaka alisema ifike wakati serikali kuheshimu viongozi wao, akifafanua kuwa aliyepita katika eneo hilo na kupewa malalamiko ya mgogoro huo alikuwa mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais ambaye kwa sasa ni Rais Samia.

Alisema Rais alitoa maelekezo kuwa wizara sita wakutane na kutatua mgogoro huo na hadi sasa maagizo yake hayajatekelezwa na mwaka umepita, akisisitiza kuwa sio jambo la busara.

"Maelekezo ya chama tunatoa mwezi mmoja mgogoro huu uishe, mamlaka zote zipo hapa za serikali. Hakuna ugumu katika kutatua huu mgogoro, kuja kwangu mmeweza kumaliza nusu ya mgogoro na haya niliyoyaelekeza nitayafikisha kwa Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo," alisema.

Shaka alisema kuwa baada ya mwezi mmoja endapo yasipotekelezwa, watalifikisha kwa Mwenyekiti wao wa CCM na watampatia ushauri wao nini cha kufanyika ili wananchi hao waishi kwa amani.

Aidha, Shaka alisema Kamishna wa Ardhi amedai wameikosesha serikali mapato kutokana na mgogoro huo, fedha ambazo zingesaidia kusukuma gurudumu la maendeleo katika nchi.

"Tunalea migogoro upande mmoja tunakutana wenyewe na upande wa pili tunahujumu nchi wenyewe kwa wenyewe, hatuwezi kwenda kwa 'style' hiyo.

"Ifike mahali tuwe na uamuzi sahihi kama eneo hili ni la mamlaka ya viwanja vya ndege basi ijulikane hivyo, kama wananchi wanastaili kupatiwa haki yao wapatiwe, mbona hakuna jambo kubwa huu mgogoro ni mwepesi," alisema Shaka.

Alisema kwa maelezo aliyoanza kusikiliza juzi na jana kuhusiana na mgogoro huo hata huo mwezi mmoja aliowapatia anaona ni muda mrefu kwa sababu vielelezo vyote vipo.

"Historia ya hili eneo mnalo na inajulikana mnakwepana, mwingine anaingilia huku na mwingine anapenya huku, tunataka kero za wananchi zimalizwe kwa wakati," aliagiza.

Mbunge wa Mtwara Mjini (CCM), Hassan Mtenga, alisema wananchi wameanza kuisha kwa siku nyingi katika eneo hilo na lipo kanisa limejengwa tangu mwaka 1953 na sio kweli kuwa wamevamia.

Alisema mamlaka yenye dhamana ya viwanja vya ndege ina eneo lingine ambalo ni pori kubwa, hivyo waangalie namna ya kuwasaidia wananchi hao wasiondolewe.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Julius Ndyamukama, amekubali kutoa kipande cha ardhi kilichovamiwa na wananchi katika eneo la Mtaa wa Mangamba, Kata ya Mtawanya, Manispaa ya Mtwara.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, alisema wanakwenda kufanyia kazi maelekezo waliyopatiwa na tayari amemwagiza Kamisha wa Ardhi kupima maeneo.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akiagana na wanachama wa CCM, baada ya kumaliza kikao katika Shina namba tano la Tawi la Pachoto, Kata ya Naliendere, Wilaya ya Mtwara mjini juzi. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Matibabu ya kutumia nyuki yazinduliwa

**Na Mary Geofrey**

KITUO cha matibabu ya maradhi mbalimbali kwa kutumia mazalia ya nyuki kimezinduliwa mkoani Dar es Salaam kwa lengo la kutoa tiba kwa magonjwa yaliyothibitishwa na madaktari ukiwamo wa kupooza.

Mgonjwa aliyepooza anawekwa katika chumba maalum na kuwekewa nyuki ambao wana tiba ya ugonjwa huo ili wamng'ate mgonjwa kama tiba.

Mtaalamu wa Matibabu kwa Kutumia Nyuki na Mazao yake, Dk. Musiba Kitema, akizungumza juzi wakati wa uzinduzi huo, alisema wanazindua kituo hicho kwa lengo la kutoa huduma ya matibabu kwa njia ya kisasa.

Alisema wana chumba maalum cha kumweka mgonjwa anayetakiwa kung'atwa na nyuki maalum ili apone ugonjwa unaomsumbua.

Alisema matibabu hayo yanapatikana kwenye hospitali kubwa duniani lakini utalaamu huo ni mgeni nchini na sababu kubwa ni kukosekana malighafi na utaalamu wa kuwafundisha wengine.

Alifafanua kuwa matibabu hayo yanafuata utalaamu kwa kuzingatia mazao ya nyuki na taratibu za afya zinafuata ikiwamo kutumia cheti cha daktari aliyethibitisha ugonjwa.

"Kabla ya kumhudumia mgonjwa lazima kuzingatia kila kitu ikiwa ni pamoja na uzito, wingi wa damu na vyote vinayofanyika hospitalini," alisisitiza.

Alisema pia zaidi ya asilimia 80 ya magonjwa yanayofahamika yanatibika kwa kutumia mazao ya nyuki. Vilevile, mtaalamu huyo alisema wana ekari 100 za kufuga nyuki Bagamoyo na lengo ni kufika ekari 2,000 kufika mwaka 2024.

Pia alisema wana malengo ya kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki.

Kwa upande wake, mgeni rasmi katika tukio hilo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Ubungo, Victor Mkumbo, alikipongeza kituo hicho na kusema kitakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa wilaya hiyo na mkoa kwa ujumla. Alisema amethibitisha kuwa kinatoa huduma zitokanazo na mazao ya nyuki na sio tiba asili na kusema kuwa kinachochea ukuaji wa uchumi nchini kutokana na matumizi ya mazalia ya hayo ya nyuki.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua dhidi ya wanaohujumu michikichi zichukuliwe haraka

**UPUNGUFU** wa mafuta ya kula nchini limekuwa tatizo sugu nchini hali ambayo huilazimu serikali kutumia wastani wa Sh. bilioni 500 kwa ajili ya kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Kwa mujibu wa serikali, mahitaji halisi ya mafuta ya kula kwa mwaka ni tani 500,000 lakini kiasi kinachozalishwa nchini ni tani 200,000, hivyo kufanya pengo kuwa tani 300,000 ambazo ni sawa na asilimia 60 ya uhitaji.

Kutokana na pengo hilo, serikali ilichukua hatua za makusudi ili kupata suluhisho la kudumu. Hatua kubwa iliyochukuliwa ni kuelekeza nguvu katika kilimo cha michikichi katika maeneo ambayo zao hilo linazalishwa ikiwamo mkoa wa Kigoma.

Ili kuhakikisha zao hilo linastawi na kuleta matokeo chanya, kwa maana ya uzalishaji kuwa mkubwa, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ilifanya utafiti wa mbegu aina ya Tanera na kuizalisha kwa wingi hatimaye kugawa kwa taasisi na wakulima. Mbegu hiyo ni ya muda mfupi kwa kuwa hutoa matunda baada ya miaka miwili na nusu tangu miche kupandwa tofauti na ile ya awali aina ya Dura ambayo huchukua miaka saba.

Miongoni mwa taasisi zilizolima kwa wingi zao hilo ni Jeshi la Magereza kupitia Gereza la Kwitanga wilayani Kigoma.

Kiwa mantiki hiyo, ulikuwa umebaki muda mfupi kuanza kupata mazao ya michikichi ambayo yangeanza kutengeneza mafuta na hatimaye kupunguza au kumaliza uhaba wa mafuta pamoja na kuokoa fedha zinazotumika kwa ajili ya uagizaji bidhaa hiyo nje. Fedha hizo zinazotumika kwa ajili ya uagizaji mafuta, zingetumika kwa maendeleo ya sekta zingine kama elimu na afya.

Hata hivyo, hujuma kubwa imefanyika kwa zaidi ya ekari 6,000 ambazo ni zaidi ya asilimia 80 ya shamba hilo kuchomwa moto na watu kuingiza mifugo hatua ambayo imerudisha nyuma jitihada za serikali kuondokana na tatizo la mafuta ya kula.

Akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kigoma juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alibainisha hilo na kuwaonya watu wanaohusika na hujuma dhidi ya zao hilo la kimkakati. Bila kuuma maneno, Waziri Mkuu alisema huo ni uhujumu uchumi na kuonya kuwa vitendo hivyo havitavumiliwa.

Pamoja na hujuma hizo, aliwahakikishia Watanzania kuwa kilimo hicho muda si mrefu kitamalizia upungufu wa mafuta ya kula kutokana na ubora wa mbegu hiyo ambayo hutoa matunda ndani ya muda mfupi.


Kama alivyosema kuwa serikali itachukua hatua dhidi ya wahusika wa hujuma hiyo, ni vyema vyombo vinavyohusika vikiongozwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kigoma na ile ya wilaya, vikachukua hatua na watakaobainika wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Serikali imeingia gharama kubwa katika kufanya utafiti na TARI kuzalisha mbegu hiyo na baadaye Magereza kuanza kutekeleza mpango wa kuondokana na uhaba wa mafuta, hivyo kitendo hicho kimerudisha nyuma juhudi mahsusi katika kuifanya nchi kujitosheleza kwa bidhaa hiyo. Waziri Mkuu, kama alivyosema, kitendo hicho ni uhujumu, hivyo hatua zichukuliwe.

Tanzania inakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo uhaba wa vyumba vya madarasa na madawati katika shule za msingi na sekondari. Jambo la kujiuliza kama zaidi ya Sh. bilioni 500 zingeokolewa kwa mwaka, ni madawati mangapi, mathalan, yangenunuliwa?

Hatua dhidi ya watu hao zichukuliwe sasa ikiwamo adhabu kali kwa watakaobainika pamoja na kutaifishwa kwa mifugo itakayokamatwa kwenye mashamba ya michikichi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




WASICHANA WENYE MATATIZO YA VIUNGO NAO WAKUMBUKWE WANAPOKUWA KATIKA HEDHI

## Muungwana Lazima Nilonge

### Kila mmoja atoe elimu ya umuhimu wa sensa



Na Sabato Kasika

**SENSA** ya watu na makazi, inatarajiwa kufanyika Agosti, mwakani, ili kupata takwimu sahihi za Watanzania ambazo zitasaidia serikali kupanga shughuli za maendeleo.

Wakati maandalizi ya sensa hiyo yakiendelea, CCM inajipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kushiriki katika sensa, ili kila Mtanzania atambue kuwa ana haki ya kuhesabiwa.

Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo ndiye anayesema hayo na kufafanua kuwa serikali ina utaratibu wa kufanya sensa kila baada ya miaka 10, kwa lengo la kupata takwimu za watu, ili ziisaidie katika mipango hiyo.

Binafsi ninaona mkakati huo wa CCM wa kutaka kutoa elimu kwa Watanzania kuona umuhimu wa kushiriki katika sensa kuwa unaweza kuleta matokeo chanya iwapo utatelezwa maeneo yote nchini.

Inadaiwa kuwa baadhi ya Watanzania huwa hawataki kuhesabiwa kutokana na sababu wanazojua wenyewe bila kujali kwamba, takwimu zao ndizo zinazosaidia serikali kupanga shughuli za maendeleo. Kwa mtazamo wangu ni kwamba, bila serikali kujua idadi ya watu wake, inaweza ikashindwa kupanga na kupeleka maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini, kutokana na kukosa takwimu sahihi za idadi ya watu.

Ikumbukwe kuwa kadri miaka inavyokwenda, ndivyo idadi ya watu nchini inazidi kuongezeka, hivyo ninadhani kwamba, suala la kujua wamefikia wangapi ni la muhimu kwa maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

Kwa mfano katika sensa ya mwaka 1967, idadi ya Watanzania ilikuwa ni watu 12,313,054; Tanzania Bara watu 11,958,654 na Zanzibar 354,400, lakini sensa ya mwaka 2012, walifikia 44,929,002, kati yao 43,625,434 wakiwa wa Tanzania Bara na 1,303,568 Zanzibar.

Hiyo inaonyesha ni jinsi gani idadi inaendelea kuongezeka kadri miaka inavyokwenda na kuifanya serikali izidi kujipanga upya na kuandaa mikakati ya maendeleo kulingana na wingi wa watu.

Idadi hiyo ya Watanzania ilitolewa na Rais wa Awamu ya Nne Dk. Jakaya wakati akizundua matokeo ya awali ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 huku akisema Tanzania ina kasi kubwa ya ongezeko la watu.

Kutokana na kasi hiyo, akatabiri kuwa hadi kufikia mwaka 2016 kungekuwa na jumla ya watu milioni 51, na akashauri kuwapo uzazi wa mpango, vinginevyo hali ya maisha itazidi kushuka, na ushindani katika rasilimali chache zilizopo utazidi kuwa mkubwa.

Hapo ndipo unapokuja umuhimu wa kuhesabiwa ili kila Mtanzania ajulikane kwa lengo la kusaidia serikali kuwa na takwimu sahihi ambazo zitaiwezesha kuandaa mipango ya maendeleo.

Kwa maana hiyo, suala la elimu kwa Watanzania kwa ajili ya kujua umuhimu wa kushiriki katika sensa, ni vyema likashirikisha watu wa kada zote, ili isambae kwa wingi kabla ya siku ya kuhesabiwa.

Itapendeza kama vyama vyote vya siasa, asasi za kiraia na watu wengine kama kila mmoja kwa nafasi yake atashiriki katika utoaji wa elimu ili asiwepo mtu ambaye hatahesabiwa bila sababu ya msingi. Ninaamini kuwa, elimu ikitolewa kwa wingi, Watanzania wote wakahesabiwa, matokeo ya sensa yatawasaidia watunga sera na viongozi kwa ajili ya kufanikisha mipango ya maendeleo na malengo ya kitaifa na kimataifa.

Kimsingi, takwimu za matokeo ya sensa huwa zina maana kwamba serikali ianze kujipanga kwa ongezeko la watu na jamii, lakini pia jamii kwa upande wake nayo ianze kujipanga kukabiliana na matokeo ya sensa.

Pamoja na hayo, sensa ina umuhimu hata kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo inagusia ajenda za maendeleo ya kitaifa, kwa lengo la kufikia maisha ya hali ya juu ya watu.

Maisha hayo hayawezi kufikiwa iwapo idadi ya watu haijulikani, kwani ili kufikia dira hiyo, Tanzania imejiwekea malengo ambayo ni ubora wa maisha, kujitosheleza kwa chakula na uhakika wa chakula, elimu ya msingi kwa wote, usawa wa kijinsia, huduma bora za afya ya msingi kwa wote.

Hayo yote yanahitaji serikali kuwa na takwimu sahihi za watu ambazo zinatokana na kila mmoja kuhesabiwa, hivyo wito wangu ni kwamba kila mmoja atoe elimu ya umuhimu wa sensa wasiachiwe CCM tu.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Samia ameonyesha uwezo, mwaka 2025 twende na mwanamke urais



Na Pascal Mayalla

Kama ni malipo, ningetengeneza fedha nyingi zaidi kama ningefanya kazi za uanasheria lakini baada ya kuhitimu shahada yangu nimeiweka tu kabatini na kuendelea na uandishi wa habari.

BAADA ya Rais Samia kuwaandaa Watanzania kisaikolojia kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kwamba tujiandae kumchagua rais mwanamke, hoja hiyo imezua mjadala mkubwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuwa ametangaza kugombea!.

Ni kwa ile kauli ya Rais Samia kwamba "Rais mwanamke tutamweka madarakani mwaka 2025. Wameanza kutuchokoza kuandika kwenye vijigazeti kwamba Samia hatosimama, nani kawaambia?"

Kwa vile mimi ni mwandishi wa habari na fani hii ni miongoni mwa fani za kazi za wito (noble profession) kama ualimu na udaktari, si kazi zenye malipo makubwa mazuri bali ni kazi kubwa yenye malipo duni, hakuna mtu anayependa umasikini, hivyo kwa waandishi wa wito, tuko kwenye fani si kwa kutafuta pesa, bali kwa sababu ya wito na mapenzi ya dhati. Wako waandishi wengi wana uwezo mkubwa na wangeweza kwenda kwenye uofisa uhusiano ambako kuna malipo mazuri, lakini wamesalia kwenye vyumba vya habari kwa sababu ya mapenzi tuu.

Mfano mzuri ni mimi mwenyewe. Licha ya kusomea uandishi wa habari, ni msomi wa sheria, mwenye shahada ya fani hiyo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kama ni malipo, ningetengeneza fedha nyingi zaidi kama ningefanya kazi za uanasheria lakini baada ya kuhitimu shahada yangu nimeiweka tu kabatini na kuendelea na uandishi wa habari.

Japo vyombo vya habari Tanzania kwa sasa tunapitia kipindi kigumu, sisi waandishi wa wito tunaendelea kuandika hata ikibidi na familia zetu kulala njaa, bado tu tunaendelea na kazi hii kama "kozi mwana mandanda, kulaa njaa kupenda."

Kwa hiyo sipendi kabisa kumsikia kiongozi yoyote, akiwadharau waandishi wa habari

Kwa maoni yangu, Rais Samia hajasema kama atagombea urais hiyo 2025 lakini pia hajasema hagombei kwa sababu majaliwa ya nani atagombea si binadamu bali ni Mungu. Kitu kizuri ambacho Rais Samia amekisema ni kuwaandaa Watanzania kumchagua Rais Mwanamke kwa sababu urais wa sasa wa Samia ni urais wa kudra za Mwenyezi Mungu.

Machi, 2015 katika mtandao wa Jamii Forums, niliandika kuhusu Rais mwanamke Tanzania kwamba: "Leo ni Siku ya Wanawake Duniani, katika safari ya kuelekea usawa wa kijinsia, Tanzania tuna wanawake wengi wenye sifa na uwezo, lakini wamenyimwa fursa za kushika nafasi za juu kisiasa kutokana na nafasi nyingi kuhodhiwa na wanaume katika muendelezo wa 'mfumo dume'.

Katika makala hiyo nilisema tuwatathmini wanawake wanasiasa watano wakubwa Tanzania kwa wakati huo na nafasi walizo kuwa nazo. Nilihoji je, wamefikaje hapo, kwa kupanda wenyewe kwa sifa, uwezo na vigezo, au wamebebwa ndipo wakafika hapo? Je, wana sifa za urais?

Wa kwanza katika hao alikuwa Samia Suluhu Hassan.

nilisema huyu ni miongoni mwa wanawake wachache wa shoka kutoka Zanzibar.

Ni Mjumbe wa Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Baada ya kuhudumu kwa miaka 10 kwenye Baraza la Wawakilishi, aliingia Bunge la Tanzania kwa miaka mitano na akawa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais na Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba.

Nikasema huyu anafaa kuwa Rais wa Tanzania ila ili kumwandaa ni ama aanze kwa kuwa Rais wa Zanzibar au CCM iamue kumpumzusha John Magufuli na kumkabidhi Mama Samia.

Gutrude Mongela alikuwa namba mbili katika makala yangu. Huyu alikuwa Mwenyekiti wa mkutano maarufu wa Wanawake uliofanyika mwaka 1995 Beijing, China na Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Yeye alifika kote huko kwa kuwa na sifa.

Huyu ana sifa ya urais ila kwa siasa zetu za Tanzania, 'by then she was already a spent force'.

Mwanamke wa tatu ni Anna Makinda aliyekuwa Spika wa Bunge la Tanzania.

Ameupata uspika kwa kubebwa na mbeleko ya jinsia, ukimlinganisha na Samuel Sitta aliyemtangulia. Lakini likija suala la urais nilisema Mama Makinda anauweza kwa sababu ni mtu mwenye msimamo usioyumba!. Uamuzi wa kirais hauhitaji mjadala kama wa Bunge.

Dk. Asha Rose Migiro ni mwingine katika kundi hilo. Ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa akimsaidia Ban Ki Moon. Baadaye akaja kuwa Waziri wa Sheria wa Tanzania.

Aliwahi kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kabla ya kwenda UN. Amefika huko kwa kuwa na sifa na tukija suala la urais anafaa.

Licha ya kwamba nilisema anafa, pia alijitosa urais wa Tanzania mwaka 2015 na kuingia kwenye tatu bora pamoja na Magufuli na Balozi Amina Salum Ali.

Nilitoa pongezi kwa wanawake hawa na kufuatia wengi kupata nafasi hizo kwa upendeleo uwe ni wa mbeleko ya viti maalum, au jitihada makusudi za harakati za kijinsia, kote huko ni kubwebwa

Niliposema pia kwamba ule msemo wa wanawake wakiwezeshwa wanaweza, nao ni mbeleko tu, hivyo kuelekea Oktoba 2015, ili wanawake waonyeshe uwezo kuwa wanaweza, sasa ni wakati wa hao wanawake wenye uwezo, wajitokeze hadharani tuwaone kuanzia kwenye kugombea nafasi ya urais.

Nilitoa wito kwa wanawake, wenye uwezo, uchaguzi wa 2015 jitokezeni kwa wingi hadi kwenye kugombea urais, ili hata msiposimamishwa angalau 2015 tuwe na ama makamu wa rais mwanamke au Waziri Mkuu mwanamke!.

**pascomayalla@gmail.com**
**0754270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tumuunge mkono Hangaya kwa Royal Tour



Na Joseph Kulangwa

Tulipopata uhuru, nasi tukafuata nyao zao na kuwalinda, tena kwa nguvu kubwa. Likawa kosa kuwinda mnyama holela eti kwa ajili ya kitoweo. Hapo ndipo sheria zikatungwa na kila kiungo cha mnyama kikaitwa nyara za serikali.

MIAKA mingi iliyopita, Mtanzania kula nyama ya mbogo, swala au digidigi lilikuwa jambo la kawaida kabisa. Mlipojisikia kubadili kitoweo badala ya kula ng'ombe, mbuzi, kondoo hata kuku, wazee walijisogeza pembeni tu na pinde zao na kurudi na swala.

Nyama hiyo kabla ya kuitwa nyara, ilikuwa ikiliwa bila kificho, huku nyingine ikikaushwa kwa ajili ya kuliwa nyakati zingine, ilimradi si kila siku mtu aende porini kuwinda.

Tulikuwa na utajiri mkubwa wa wanyamapori, huku tukiwinda kwa kunyang'anyana na wanyama walao wanyama wenzao, simba, chui na fisi hata duma ndio wanyama maarufu kwa kula wenzao.

Kwa mbali walifuatwa na nyoka na mijusi wakubwa kama mamba, lakini bado wanyama pori waliendelea kuwa wengi wakiongezeka kadri siku zilivyosonga mbele, hivyo hatukuwa na uhaba wa nyama.

Hata walipokuja Wakoloni, nao walionja nyamapori na kuzipenda, kidogo kidogo wakaanza kubaini kwamba wanyama hao wangetoweka, wakaja na sheria za kuwalinda.

Tulipopata uhuru, nasi tukafuata nyao zao na kuwalinda, tena kwa nguvu kubwa. Likawa kosa kuwinda mnyama holela eti kwa ajili ya kitoweo. Hapo ndipo sheria zikatungwa na kila kiungo cha mnyama kikaitwa nyara za serikali.

Kila ulipokutwa na nyama, pembe, jino, ngozi au kucha ya mnyama wa porini, basi wewe ukishindwa kujieleza kwa Pilato ni kifungo kukuhusu kama si faini ya kuua mtu.

Kumbe ulinzi huo ulikuwa wa manufaa kwamba tulitaka wawindaji wawinde kwa fedha, watazamaji watazame kwa fedha na hata wapigapicha wawapige wanyama hao kwa fedha ili tujenge uchumi wa taifa letu na tujitegemee.

Ndipo sasa dhana ya utalii ikajengeka, tukaanzisha taasisi na vyombo vya kusimamia utalii na kulinda maliasili hiyo ya wanyama. Wageni wakaja nchini kuangalia wanyama wetu kwa kulipa fedha, tena za kwao zenye nguvu nasi kufaidika.

Tumeendelea hivyo huku tukipambana na wawindaji haramu tukawaita majangili. Tukiwasaka na kuwakamata na kuwafunga miaka kadhaa ilikuwa onyo kwa wengine. Dhana kuu ikawa ni kuhakikisha wanyama hawadhuriki hawauawi, hawapotei na hawatoweki.

Kwa kulitilia maanani hilo, hivi karibuni tukamwona Mama Hangaya akifanya ziara karibu nchi nzima akirekodi vivutio vyetu kupitia safari ile ya Royal Tour sijui niite Utalii wa Kifalme! Vyovyote, Mama amefanikkiwa sana kwa hilo bila shaka tusubiri tuone alichorekodi ingawa nina uhakika kitavutia.

Watanzania tunapaswa kufuata nyayo zake sasa, kila unapoweza kutangaza utalii wetu tangaza, kila unapoweza kulinda rasilimali zetu fanya hivyo kwa ajili ya mustakabali mzuri wa Taifa hili lenye kila aina ya vivutio.

Lakini lazima tujiongeze, kweye hoteli na ndege zetu. Hivi nani alisema wageni kutoka Ulaya na Marekani wanatamani kuja kulala kwenye hoteli kama za kwao? Nani alisema wakija wanataka wale vyakula walivyoacha kwao?

Kwani mathalan katika hifadhi zote nchini tukijenga nyumba za tembe na msonge, au hata mapango wakalala humo? Hivi wenye ndege zetu tukiwapikia ugali badala ya mkate na keki au uji badala ya chai na soda, tena wa ulezi itakuwaje?

Hivi wakirudi kwao wakasimulia kuhusu utamu wa ugali wa mtama au uwele, uji wa ulezi au mchele itakuwaje, hatuoni tutakuwa tumemsaidia Mama Hangaya kutangaza taifa hili na utajiri wake?

Mimi mathalan, nikitoka Bongo nikaenda Marekani au Uingereza au Mashariki ya Mbali, bila shaka nitatamani kulala Hilton, Churchill, Dupont Plaza, Otani nakadhalika, nitatatami kula piza, baga, sushi, na kadhalika, ili nije kusimulia Wabongo.

Kama nia ni kutangaza utajiri tulionao, hamwoni ugali na uji ni utalii, si tu ngoma, wanyama, ndege, miti na majabali.

Hebu tujaribu basi, Dreamliner moja iwe ya ugali na uji tu, tuone kama utalii hautaongezeka. Tuwalaze kwenye ngozi kunako tembe na misonge tuone kama hawatasimulia.

Tutake tusitake, vitanda vya teremka tukaze ni mali sana katika medani ya utalii, vibuyu badala ya vikombe vya udongo ni mali sana katika utalii, tuamke kumekucha. Hongera sana Hangaya kwa Royal Tour, bila shaka italipa tu inshallah!

**Alamsiki!**

## SAFU

## KONA YA UKWELI

# Vyama vinavyosubiri ruzuku ndipo vifanye siasa havitufai



Na Thobias Mwanakatwe

**Na bahati mbaya hata baadhi ya vyama vinavyopata ruzuku vimekuwa na matumizi yasiyoridhisha. Tumekuwa tukishuhudia kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiviumbua kutokana na matumizi yasiyoridhisha ya fedha hizo za ruzuku.**

SERIKALI ilipoamua kuurejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, baada ya kuufuta mfumo huo mwaka 1965, moja ya taratibu zilioelezwa ni kwamba vyama hivyo vingeweza kupewa ruzuku ya kuviwezesha kuendesha shughuli zao.

Pamoja na kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ilipitishwa na kuanza kutumika rasmi Julai 1, 1992, vyama vya siasa havikupewa ruzuku hadi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 ambao ulikuwa wa kwanza tangu Tanzania ilipoingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini.

Baada ya uchaguzi huo, utaratibu wa kutoa ruzuku ulibadilishwa tena mwaka 1996 na sheria ilitaka vyama vinavyopewa ruzuku viwe vimepata zaidi ya asilimia tano ya kura katika uchaguzi mkuu. Kigezo kingine kilichowekwa na serikali ni kwamba chama husika hakina budi kuwa na wabunge.

Hata hivyo, hakuna maelezo yaliyotolewa kuhusiana na vyama kuwa na sifa hizo, kwa kiasi kikubwa sababu za kutaka vyama hivyo vitimize sifa hizo ni kutaka kuwapo na vyama makini vya siasa na si vyama vya ruzuku.

Binafsi, naamini kuwa serikali ililazimika kuweka vigezo hivyo kutokana na uzoefu iliyoupata mwaka 1995 ilipotoa ruzuku kwa vyama vyote vya siasa vilivyokuwa vimepata usajili wa kudumu kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi mkuu.

Nakubaliana kwa asilimia 100 na uamuzi huo wa serikali wa kuweka vigezo hivyo kwa kuwa ni jambo lililo wazi kuwa licha ya kwamba Tanzania tunavyo takriban vyama 17 vyenye usajili wa kudumu, vingi havionekani kama vipo.

Badhi ya vyama vimekuwa vikiibuka kama uyoga unapofikia wakati wa Uchaguzi Mkuu. Pengine vinafanya hivyo ili vipate ufadhili wa kifedha kutoka kwa washirika wao wa ndani na nje.

Baada ya uchaguzi kwisha, vyama hivyo vinapotea kabisa kiasi kwamba Watanzania wengi wanaviona kama ni vyama ambavyo viliibuka kwa lengo la kutaka kupata ruzuku ambayo inatolewa kwa vyama vilivyotimiza masharti hayo.

Utashangaa hata katika kipindi hiki baadhi ya wagombea urais wamekuwa wakilalama tu kwamba vyama vyao vinakabiliwa na ukata jambo ambalo ni kweli. Lakini unajiuliza kwa nini haviwi na mikakati ya kupata pesa ikiwamo kuanzisha miradi itakayoviingizia kipato badala ya kulilia ruzuku.

Na bahati mbaya hata baadhi ya vyama vinavyopata ruzuku vimekuwa na matumizi yasiyoridhisha. Tumekuwa tukishuhudia kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiviumbua kutokana na matumizi yasiyoridhisha ya fedha hizo za ruzuku.

Inashangaza kuona baadhi ya vyama licha ya ukongwe wake vinashindwa hata kujenga ofisi zake za kudumu na badala yake vinapangisha lakini vinapata ruzuku jambo ambalo ni fedheha kwa vyama hivyo.

Ifike wakati Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye ndiyo inavilea vyama hivyo, itunge muswada na hatimaye Bunge kutunga sheria ambayo italazimika kuvifuta vyama ambavyo haviko 'active' ili kuondokana na msululu wa vyama ambavyo havina faida na uwapo wake.

Hatuwezi kuwa na vyama vya siasa ambavyo havifanyi siasa badala yake vinavizia tu unapofika wakati wa uchaguzi mkuu ndipo vinaibuka kama uyoga na kuja na ilani zenye mambo mengi ambayo hata vikipewa madaraka haviwezi kuyatekeleza.

Vyama vinavyoibuka wakati wa uchaguzi tu ndivyo hivyo ambavyo vinakuja kuwachanganya wananchi kwa kutoa sera ambazo vinatambua ni ngumu kutekelezeka.

Japo kunaweza kukawa na hoja kwamba miaka mitano ya utawala huu havikuruhusiwa kufanya siasa, hiyo si kweli siasa ingeweza kufanyika kwa kupitia kwa viongozi wao ambao ni wabunge na kadhalika.

Umefika wakati sasa vyama vya siasa viache kufikiria na kudhani kuwa haviwezi kuishi kuendelea na majukumu yake bila kupata ruzuku inayotolewa na serikali.

**Mungu Ibariki Tanzania**

**KWA MAONI NA USHAURI TUWASILIANE mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# NAFASI YA MAWASILIANO KATIKA KUJENGA NDOA IMARA- 2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Baadhi ya Watanzania wamekuwa wakihoji kila mmoja kwa upande wake kuhusu uamuzi huo wa serikali, upande mmoja ukikubaliana na kupongeza huku upande wa pili ukikosoa.**

JUMAPILI iliyopita tuliona kuwa mawasiliano ni jambo muhimu katika uhusiano. Mawasiliano yanapokosekana athari zake ni nyingi. Hata pale mawasiliano yanapokuwapo, lakini yanapokosa nidhamu na utaratibu, huweza pia kuharibu uhusiano.

Mawasiliano huwezeshwa na kiungo kinachoitwa ulimi ambao ni chombo cha mawasiliano. Ulimi wa mtu unaweza kuwa dawa na sumu kwa wakati mmoja. Ulimi hutumika kumwabudu Mungu, na wakati huo huo hutumika kulaani na kunena mabaya dhidi ya wanadamu wenzetu.

Ndoa nyingi zimevurugika kwa kutumia vibaya ulimi. Wengine wamewasema wenzi wao vibaya na kuwashambulia kwa maneno yaliyochoma na kuumiza mioyo yao. Wengine wametwezwa na kudhalilishwa kwa maneno na majina mabaya.

Katika sehemu hii ya pili, tutajadili jinsi ya kuimarisha mawasiliano katika ndoa. Kama ndoa haina mawasiliano, inabidi kuchukua hatua za kubadili hali hii. Kwani kama hakuna mawasiliano kwenye uhusiano, hata amani na upendo navyo vinakuwa havipo.

Ili kuwa na mawasiliano mazuri katika ndoa ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

**Kujifunza**

Kujifunza ni suala ambalo mtu anaweza kuwa nalo. Kama wanandoa hawana mawasiliano kwenye uhusiano wao, wanaweza kuanza kujenga tabia ya kuwasiliana. Kama kila wanapotaka kufanya mawasiliano wanashindwa kufikia muafaka na kuishia kugombana, wanandoa wasikate tamaa.

Jambo la msingi hapa inabidi kuahirisha mazungumzo na kuyarudia baadaye wakiwa katika hali nzuri zaidi. Ni busara kuzingatia kuwa, kushindwa kufikia mwafaka kwenye jambo fulani isiwe chanzo cha kuvunjika kwa mawasiliano.

**Kutoogopana**

Wanandoa hawahitaji kuogopana bali kuheshimiana na kupendana kwani penye woga upendo hauwezi kustawi. Woga ni adui wa mawasiliano. Mume na mke hawawezi kuwasiliana ipasavyo kama wanaogopana. Mawasiliano yanakuwa na maana pale kila mmoja anapokuwa huru kwa mwenzake. Uhuru huu hauwezi kuwapo katika mazingira ya woga. Wanandoa wajenge mazingira ya kuheshimiana na kupendana. Tengeneze mazingira ya mwenzako kuwa huru na wewe.

**Kusikiliza**

Mawasiliano hayawezi kuwapo kama watu hawako tayari kusikilizana wanapozungumza, yaani kusikiliza kwa makini. Mara nyingine, unakuta mtu anapozungumza, mwenzake huwa anafikiria maneno ya kujibu baada ya yeye kumaliza. Mtu anasubiri mwenzake azungumze hadi afike mwisho, halafu mara moja unakuta anarukia wazo. Lakini wakati alipokuwa anangojea mwenzake amalize usemi wake, hakuwa anasikiliza. Mwingine unakuta mwenzake anaongea yeye anashughulika na simu yake.

Mwanandoa anapotaka mawasiliano mazuri katika ndoa yake, lazima kujifunza kuwa msikilizaji mzuri wa mwenzake wakati wa mazungumzo. Inabidi kujifunza kwa sababu watu wengi hawajui jinsi ya kusikiliza, kwani sehemu kubwa kwenye mazungumzo, mtu hupenda kulinda nafsi yake, heshima na hadhi.

Katika mazingira haya, kuwasikiliza wengine huwa ni ngumu. Kusikiliza huenda sambamba na kusubiri. Kusikiliza huleta ufahamu. Usipende wewe kusikilizwa tu, lakini nawe pia penda kusikiliza wengine.Hivyo, jifunze kumsikiliza mwenzi wako (learn to listen). Mpe muda wako na masikio yako.

**Majukumu**

Katika jamii nyingi za Kiafrika, majukumu ya wanawake na wanaume karibu ni yale yale. Mama ni mlezi na mwangalizi wa nyumba na baba ni mtafutaji. Jambo hili bila shaka ni la kimaumbile, kwamba mwanamke nafasi yake ni kuangalia familia kwa karibu zaidi (hata kama ameajiriwa au amejiajiri). Nyumba ni mwanamke. Mambo yakienda vizuri au vibaya nyumbani, inabidi kuangalia mwanamke amesimamaje katika nafasi yake.

Kwa upande wa mwanamume, nafasi yake ni kuhangaikia familia hata kama hana anacholeta. Hata hivyo, maandiko matakatifu ya Mungu yanasisitiza kuwa, jukumu la kulea na kutunza familia ni jukumu la wote wawili kwa pamoja, yaani mume na mke. Kila mmoja ana nafasi na wajibu wake katika suala zima la malezi ya watoto.

Ni muhimu ikaeleweka kwamba, baada ya kupatikana watoto ndani ya nyumba na shughuli za kutafuta huongezeka kwa sababu kuna familia kubwa, mama na baba hujikuta wakiwa wametingwa sana na majukumu. Kutingwa huku kusipoangaliwa kwa makini, kunaweza kusababisha mawasiliano kati ya wanandoa kuharibika.

**Itaendelea Jumapili ijayo**

- **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

SEPTEMBA 19, 2021
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


**Utamu wa juisi ya limao**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Mambo muhimu kuwekeza katika ujenzi wa nyumba



**HARUSI**

Ukurasa 12




**KUCHA ZINAZOSEMA**

# Zinakamilisha urembo wa mwanamke

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | B | I | S | H | A |
| | W | | | O | |
| D | A | I | | D | |
| | N | | B | A | I |
| | G | | | R | |
| M | A | U | T | I | |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
GEA, OKA, LAUMU, SWALA, LEGEVU, SUKUMA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Alichokifanya daktari

MTOTO John alikuwa anamsaidia mama yake kuwandaa samaki kwa ajili ya kitoweo cha usiku. Wakati akiwaondoa magamba alianza kumuuliza mama yake.

**John:** Mama kwani samaki wanalia?
**Mama:** Mi sijui mwanangu
**John:** Wanatoa machozi kama sisi?
**Mama:** John usinisumbie, yote hayo sifahamu
**John:** Mbona watu wanasema kilio cha samaki machozi huishai majini?
**Mama:** John huo ni msemo tu, unamaanisha hakuna mtu anayejua kiasi unachoumia pale unapopatwa na jambo.

**SWALI**
Mikoa gani ya Tanzania inasifika kwa kilimo cha chakula?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Dalili za mtu kuchukuliwa nafasi yake

KARIBU tena msomaji tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita tuliona siri kwa nini cheo au nafasi ya mtu huchukuliwa. Leo tuangalie dalili za kutolewa kwenye nafasi.

Wako watu ambao kazi yao ni kufanya shauri la kukuangusha. Hii ikimaanisha kwamba yapo mashauri yanayoendelea katika ulimwengu wa roho ambayo wewe huelewi kwenye vikao vyao vya siri. Na hiyo imelenga kukuangusha tu utoke kwenye ndoa yao au kazi au biashara yako.

Unaweza kuangushwa utoke kwenye cheo chako. Unashangaa haupo tena kama zamani, huwezi kufanya kazi tena kama zamani. Dalili ya kutolewa kwenye nafasi yako huwezi kuwajibika kama zamani.

Kama ni mwana maombi unajikuta huwezi kufanya maombi kama zamani. Hiyo tayari umeshaondolewa kwenye nafasi yako, umebakia nakala haupo pale ulipotakiwa. Faida au nguvu yako ipo pale ambapo Mungu anataka. Kama haupo hapo, wewe ni sawa na nakala (photocopy).

Unashangaa umebadilika, kumbe tayari umetolewa. Usipokaa kwenye nafasi yako, watu wengine watakaa hapo. Usipochukua nafasi yako, wengine watakupokonya. Ukizembea watakutoa na ukishatolewa, watafurahia. Wapo watu wametolewa na hawajui ni kwa nini.

Lazima ukae kwa mamlaka kwa sababu kuna roho zinaondoa watu. Usipokaa imara kwenye nafasi yako, mwingine ataikalia nawe ubakie unashangaa. Na Mungu anapotaka kukubariki anaangalia, je, upo kwenye nafasi yako?

Siku zote usifikiri unapowekwa kwenye nafasi fulani ni heshima ndogo. Nafasi yoyote ile unayopewa ndio baraka zako zilipo hapo. Unaposikia mtu anasema, "mimi naacha kazi", siyo kwa akili yake, kuna watu walishamtoa kitambo.

Msomaji wangu, hebu angalia familia ambayo mama kachukua nafasi ya mumewe. Hiyo familia haina baraka. Wapo wanawake ambao wao ndio waongeaji kwenye ndoa.

Utasikia, baba fulani unasemaje? Tumpe hizi Sh. milioni moja au tumpe hili gari? Baba anajibu; muone mama bana, akisema ndiyo tumemaliza. Ukiona hivyo, baba tayari ametolewa kwenye nafasi yake, hana nguvu ya uamuzi. Vituko vya aina hii ni vingi kwenye maisha ya kila siku.

Ziko familia zingine mama ana sauti kuliko baba. Kitu mama akisema watoto wanatekeleza. Lakini baba akisema, watoto wanampuuzia. Hapo baba kashatolewa kwenye nafasi yake kama mkuu wa kaya. Mwanamume anapotolewa kwenye nafasi, hiyo familia inakuwa na shida.

Wakati mwingine unaweza kutolewa kwenye nafasi lakini hujui. Ni kwa sababu akili yako inakuonyesha ni wewe umetoka mwenyewe kumbe umetolewa. Na walipokutoa, mashauri yao yametimia. Ni muhimu sana kuombea nafasi uliyonayo ili isichukuliwe.

Kila mtu anapaswa kuheshimu nafasi ya mwenzake. Kuna mahali ukiingia, sekretari ana nguvu kuliko mkurugenzi wake. Ndiyo maana unakuta watu wanatumia nafasi zao kama ni mabinti, kuwarubuni mabosi kwa namna mbalimbali, ikiwamo uhusiano.

Hivyo, chunga nafasi yako. Mungu huwa anasisitiza kwamba shika sana ulicho nacho asije mtu akatwaa taji yako. Taji ni nafasi yako, kazi yako. Ukipewa nafasi kaa kwa ujasiri. Onyesha nafasi hiyo ni yako na watangazie watu kuwa, "hii ni nafasi yangu".

> **Msomaji wangu, hebu angalia familia ambayo mama kachukua nafasi ya mumewe. Hiyo familia haina baraka. Wapo wanawake ambao wao ndio waongeaji kwenye ndoa.**

Kama nilivyoeleza awali kwamba wapo watu hufanya mipango kwa mashauriano kwenye vikao vya siri ili kuwaondoa wenzao kwenye nafasi zao. Na ukishaondolewa kwenye nafasi dalili ni hizi; huwezi kufanya kazi kama ulivyokuwa zamani. Hiyo ni kwa sababu nguvu ipo kwenye nafasi. Ukitoka hutakuwa na nguvu ile ile.

Ukiwa kwenye nafasi unakuwa na uwezo, mamlaka, lakini ukitoka, vyote hivyo navyo huondoka na kubaki wa kawaida. Hiyo ni kwa sababu cheo au nafasi yako kwenye ulimwengu wa roho imeshaondolewa.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kuhusu dalili za mtu aliyechukuliwa nafasi au cheo chake. Hii ni vita ambayo imejikita sana maofisini na hata kwenye ndoa nyingi.

Wiki ijayo nitatoa mifano kadhaa ya watu walioondolewa kwenye vyeo au nafasi zao pasipo kujua, na hata pale wanapogundua, wanabaki kushangaa kwani maji yakishamwagika hayazoleki tena! Maisha Ndivyo Yalivyo.

***Je, una maoni au kisa cha kimaisha ambacho ungependa tujadili pamoja kiwafumbue macho wengine? Ukiwa tayari tuma ujumbe mfupi kupitia simu ya kiganjani 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Machinga kupangwa sawa lakini suluhisho la kudumu muhimu

HIVI karibuni Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, alisema zaidi ya wafanyabiashara 45,000 Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitano hadi sita, wameandika barua za kufunga biashara zao lakini kwa uchunguzi wao, wengi walikwenda kuwa machinga.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kukwepa mfumo rasmi wa kulipa kodi na kufanya biashara zao kama machinga, huku wengi wakikwepa utaratibu huo kwa kuwa wanajua watatakiwa kuwajibika kulipa kodi.

Meya Songoro alisema kwa Manispaa ya Kinondoni kuna zaidi ya wafanyabiashara 9,000 walioandika barua za kuomba kuondoka kwenye mfumo rasmi kwa madai kuwa hakuna biashara lakini walivyofuatilia, baadhi yao walirudi kuwa machinga.

Kwa sasa idadi ya machinga inaongezeka kiasi cha kusababisha wenye maduka kushindwa kufanya biashara kwa kuwa machinga wanapata wateja wengi zaidi yao kutokana na ukweli wananunua bidhaa kwa bei ya jumla na kuuza rejareja.

Wengi wamefika mahali kuona bora wawe machinga na baadhi wanamiliki vibanda ambavyo wakati mwingine ukipiga hesabu ya bidhaa zilizopo ni sawa na duka dogo, ila kwa kuwa hawalipi kodi basi wanaendelea kusambaziana taarifa.

Athari ni kubwa kwa serikali ambayo haiongezi idadi ya wafanyabiashara wanaokuwa kwamba wakifanyiwa tathmini mwaka jana ni tofauti na mwaka huu kwamba unaonekana ukuaji wa biashara yake.

Nyingine ni kuongeza idadi ya watu wanaokimbilia mjini kwa kuwa wanasambaziana taarifa kuwa biashara hiyo inalipa na hakuna vikwazo vikubwa kwenye kuifanya.

Athari nyingine ni mji au jiji kukosa mwonekano mzuri kwa kuwa bidhaa za kila aina hupagwa kila mahali kiasi kwamba hata kazi iliyofanywa na mipango miji haina thamani yoyote.

Pia halmashauri zinapoteza mapato mengi yatokanayo na masoko kwa kuwa wafanyabiashara wengi wanakuwa nje ya soko lenye mfumo rasmi na wanauza bidhaa zile zile zinazouzwa na wale wanaolipa ushuru, ambao husaidia kupata fedha za utekelezaji wa shughuli za kijamii kama elimu, afya, maji na moundombinu.

Tangu Rais Samia Suluhu Hassan, awatake wakuu wa wilaya na mikoa kushirikiana kupata namna nzuri ya kuwapanga wafanyabiashara hao, nimeona kasi ya mapango ya onyo kuonyesha eneo lisilofaa kufanyabiashara yanaongezeka.

Niliwahi kuandika katika safu hii kuwa bila kuwapanga wafanyabiashara hao hali itakuwa mbaya na serikali itaendelea kupunguza idadi ya wafanyabiashara wanaotambuliwa na mifumo rasmi ya kikodi.

Ni muhimu kufuatilia hawa wanaoitwa machinga kama ni machinga kweli kwa wapo wenye biashara zenye bidhaa nyingi kama duka au kibanda lakini kwa kuwa yuko eneo la muda basi anahesabika ni machinga.

Wakati huu wa kuwapanga ni muhimu kujifunza nchi zingine zimefanyeje kwa kuwa ziko zilizofanikiwa kuwapanga katika maeneo sahihi, ikiwamo kuwazoesha wananchi kwenda hayo maeneo kununua bidhaa, tofauti na hali ilivyo sasa machinga wanawafuata na kuziba hata njia za watembea kwa miguu.

Maeneo mengine ni ya kupita magari wao wamegeuza ndiyo eneo la biashara kiasi kwamba hakuna usalama wao na watembea kwa miguu na hali huwa mbaya zaidi kuanzia saa 12 jioni kwa kuwa vibanda vinavyotembea vyenye bidhaa nyingi hupangwa maeneo hayo.

Muhimu zaidi ni kuboresha huduma za kijamii kama miundombinu na umeme vijijini ikiwamo kuimarisha shughuli za kibiashara, ili wengi waone uwezekano wa kuzalisha na kuuza huko waliko kuliko kila mmoja kutaka kwenda mjini.

Ikiwa vijijini kutakuwa na miundombinu sahihi, mzunguko wa fedha na huduma muhimu kama afya maji na elimu naamini wengi watapenda kubaki kwenye maeneo yao ambako maisha ni rahisi zaidi kwa kuwa ana uhakika wa kulima au kununua kwa bei rahisi, haishi kwenye nyumba ya kupanga na hatumii nauli.

Pia ni muhimu kuimarisha masoko ya vijijini ili watu wakanunue na kuuza huko huko, hasa kujifunza nchi zilizoendelea zimewezaje kuendeleza miji yake midogo kiasi cha wengi kupenda kuishi huko kuliko kila mmoja kutamani kukimbilia mjini.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI



Septemba 11, mwaka huu ilikuwa ni siku ya furaha kwa Christopher Mahende na Gapi Matata baada ya kutimiza miaka 10 ya ndoa yao , iliyoambatana na sherehe ya aina yake Ulongoni jijini Dar es salaam.







# MITINDO

## MET GALLA 2021









# Mastaa walivyotoka kipekee


JIJI la New york nchini Marekani, lilitawaliwa na kila aina ya mavazi katika usiku wa shindano la maonyesho ya mavazi linalofahamika kama Met Galla.

Katika maonyesho hayo yaliyofanyika siku ya Jumatatu, wasanii mbalimbali walishindana na mavazi ya kipekee na kuibua shangwe za kila aina.

Baadhi ya wasanii walioonekana kutia fora ni mwanamuziki Lil Nas, Marilyn Monroe, Grace Kelly, Rihanna, Barbie Ferreira, Yara Shahidi na mtoto Biblie Eilish.

Hawa ni baadhi ya mastaa walivyojimwaga katika tamasha hilo wakiwa na mavazi tofauti.

UREMBO



KUCHA ZINAZOSEMA

# Zinakamilisha urembo wa mwanamke

KUCHA ni moja ya kiungo kinachoweza kuelezea kwa urahisi uzuri na urembo wa mwanamke.

Hata hivyo, ili kuwa na mwonekano mzuri wa kucha, ni lazima kuziweka katika hali bora kila wakati.

Kutokana na umuhimu wake, leo nitakupa hatua mbalimbali za utunzaji wa kucha kwa ajili ya kunogesha urembo wako.

Kwanza unatakiwa kuwekeza kwenye vifaa vya kisasa vya kutunzia kucha. Tumia brashi ya kucha kwa kusugua chini ya kucha na kutoa uchafu sehemu ngumu ambayo unajilundika. Pia unaweza kutumia mswaki ukiwa hauna vifaa vya kisasa.

Tumia maji ya moto na sabuni ya kunawia mikono, anza kwa kusugua chini kabisa kwa kushikilia brashi na sugua kuanzia nyuma na kwenda mbele taratibu, kisha juu ya kucha kwa kuzunguka.

Toa rangi kwa kuloweka pamba kwenye polisi 'remover' na sugua kwa vidole vyenye hinna na huna haja ya kuitoa.


Kuweka vidole vyenye afya na nguvu, vipumzishe kwa kutumia polishi kila baada ya wiki kadhaa.

Loweka kucha na maji kwenye bakuli na sinki, kifaa cha uwezo wako hata kama ni beseni, kwa maji ya moto ya uvuguvugu na pitisha sabuni ya kunawia mikono. Usiloweke mkono mzima, kwa dakika tatu kwenye maji ili kufanya mikono kuwa mikavu.

Baada ya hapo suuza kwa maji safi ya uvuguvugu au yaliyokuwa kwenye chombo.

Unaweza kutumia kifaa cha kukatia kucha au kifaa cha kupunguza kuweka sawa kama hautazikata.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Utamu wa juisi ya limao



JUISI ya Limao na Tangawizi ni kinywaji rahisi kuandaa na kizuri kwa afya kutokana na kuwa na virutubishi mbalimbali.

Unaweza kunywa juisi yake wakati wowote kuanzia asubuhi baada ya kupata kifungua kinywa, mchana na usiku kabla ya kulala.

**MAHITAJI**

Malimao freshi sita, asali kikombe kimoja, tangawizi iliyokwanguliwa nusu kikombe, maji ya kuchemshia vikombe viwili na maji baridi vikombe 14.

**NAMNA YA KUANDAA**

Chukua bakuli safi, kwenye kamua malimao kisha toa mbegu zote, yabaki maji ya limao.

Washa jiko, bandika sufuria, weka vikombe viwili vya maji, asali na tangawizi. Acha mchanganyiko uchemke kwa moto mdogo kwa muda wa dakika 10, mpaka asali iyeyuke na harufu nzuri ya tangawizi isikike.

Epua na acha ipoe. Chukua jagi safi weka maji ya limao, maji ya baridi vikombe 14, kisha weka mchanganyiko uliotoa jikoni. Changanya vizuri na kisha weka kwenye jokofu kwa muda wa saa moja.

Kama utapenda weka majani ya mnanaa na giligilani ili kupata harufu nzuri.

Juisi yako itakuwa tayari kwa kunywa wakati wote utakaojisikia.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Mambo muhimu kuwekeza katika ujenzi wa nyumba





UJENZI wa nyumba ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine wowote. Ni vigumu sana kufanikisha kuwa na nyumba ya ndoto yako endapo hujaweka mipango mizuri ya kuwekeza pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo unayoitamani.

Mtaalamu wa ujenzi, Khamis Ally, anasema viko vitu ambavyo mtu ambaye amekusudia kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba anapaswa kuvifahamu.

Moja ya vitu hivyo anasema ni kuweka mipango madhubuti juu ya ujenzi wa nyumba katika mtazamo wa sasa na wa baadaye.

"Unapopanga kujenga nyumba yako ni muhimu kuiona baadaye na mabadiliko yake. Ni vema ujue jengo lako litakavyokuwa kabla ya kuanza ujenzi, ufahamu uzuri wake, ukubwa, rangi.

"Ujue ni wapi utakwenda kununua saruji, mbao, nondo na vinginevyo. Umfahamu fundi atakayekujengea, ukanda unaojenga ni wa aina gani kijiografia na ufahamu kama eneo lako halina mgogoro wowote iwe ni kwa upande wa serikali au majirani," anasema.

Jambo lingine ambalo mtaalamu huyu anashauri ni kujenga nyumba inayokidhi mahitaji yako. Pia anasema ni muhimu kufahamu ni nyumba ya aina gani unayotaka kujenga kwa kutazama mahitaji yako katika uhalisia wa sasa na wa baadae na kumshirikisha mtaalamu aliyebobea katika usanifu wa nyumba za kuishi.

"Kujenga kwa kuzidi mahitaji yako kunaweza kuleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi. Unaweza ukajiuliza maswali kadhaa, Je, kuishi kwenye hiyo nyumba kuna faida zaidi kuliko kupanga? Ni muhimu kuhakikisha kwamba unajenga kwa faida na si hasara.

"Baadhi wamejikuta wamejenga nyumba ambayo inadumu kwa muda mfupi. Wako waliofikiri kutumia vifaa duni vyenye gharama ndogo ndiyo namna ya kupunguza gharama na badala yake walijikuta wakihitajika kuvibadili baada ya muda mfupi na kwa gharama kubwa zaidi.

Pia wako waliochakachua kwa kujua kwamba ndio njia nzuri ya kupunguza gharama, na kujikuta katika hatari za nyufa, kubomoka na kutokudumu kwa muda unaofaa. Hakikisha unakuwa na mtazamo wa kiuchumi wa kujenga kilicho bora, imara, kinachodumu na kwa gharama nafuu," anaongeza.

Ally anasema kwamba kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba, ni vizuri pia ukadodosa na kupata taarifa sahihi zinazohusiana na ujenzi zikiwamo gharama ambazo hutumika kulipa mafundi, vifaa vinavyopaswa kununuliwa ili kukusaidia kufanya uamuzi bila hofu na usionekane hujui chochote mbele ya mafundi wako na wakatumia mwanya huo kukudanganya baadhi ya vitu.

Anashauri pia kuhakikisha unasimamia ipasavyo ujenzi wa nyumba yako unapoanza hadi unapomalizika ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa badala ya kuwaacha huru mafundi.

## Dondoo namna kuchagua matandiko kitanda cha mtoto



WAZAZI wanapokuwa na mtoto jambo la kwanza wanalozingatia ni kupata kitanda chenye matandiko mazuri. Mbali na mwonekano mzuri wa kitanda lazima kuwapo na mwonekano mzuri wa shuka anazolalia.

Hizi ni baadhi tu za dondoo za kuchagua matandiko kwa ajili ya mtoto mchanga.


**1:** Chagua matandiko kulingana na hali ya hewa ya wakati husika, ni lazima kujua kipindi cha majira ili mtoto wako weze kulala sehemu salama.


**2:** Nunua tandiko lilotengenezwa kwa pamba, kwani bei yake ni rahisi na inampa joto wakati wa barini na kipindi cha joti anapata ubaridi. Matandiko ya pamba yanamfanya mtoto kujisikia furaha na ngozi yake kuwa katika hali bora zaidi.

**3:** Matandiko ya Polyster inapendeza zaidi yanapokuwa kitandani, gharama yake ni nafuu kuliko pamba lakini si bora sana kutumia mtoto kutokana na kuwa na hali ya joto na kumfanya atokwe na jasho.

**4:** Matandiko ya sufi, haya ni mazuri sana kipindi cha baridi kutokana na uwezo wake mkubwa kuzalisha joto. Ni muhimu wakati unaponunua hakikisha utatumia katika kipindi hicho na si vingine.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
!
VIOO-NGOZ
BAADHI
AFIRIKA
Si Si


NDANI YA KIBASI
JAPO NNA SHUGHULI LAKINI JICHO LANGU KWA LEO LIPO KWAKO
SURA MBOVU KWA ROHO MBAYA! KILA MTU AFANYE YAKE TUSIWANGIANE!
NIKISHINDA AU NIKI-FUNGWA HAYAKUHUSU! UMBEA WA NINI?
MBONA POVU?
NAMFURAHIA DOKTA ANAYE-TAKA CHANJO IWE LAZIMA AU NYIE MNAONAJE?
KAMA USHA-FIKA SHUKA!
DEREVA JAZA SAUTI YA SINGELI
KAMA HAJACHANJA MWAMBIE SIE TAYARI
NAHISI BARIIIDI!
SIJIELEWIELEWI HOMA IPO JUU MARA IPO CHINI!
USIWE NA PRESHA HATA 'UKIGONGWA' NYINGI MNYAMA HATOSHUGHULIKA YUPO BIZE LEO
DOKTA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...VUMILIA MAUMIVU UPATE RAHA YA PEPONI

## Wanajeshi wavamiwa, 10 wauawa Cameroon

**Bamenda, CAMEROON**

MVUTANO umeongezeka katika eneo la Kaskazini-Magharibi mwa Cameroon sehemu ambayo doria ya kijeshi imeshambuliwa na askari 10 wa serikali kuuliwa.

Shambulio hilo lilitokea Alhamisi iliyopita mashariki mwa mji wa Bamenda. Hakukuwa na taarifa rasmi kuhusu suala hilo, wala hakuna ripoti iliyotolewa. Lakini karibu wanajeshi kumi waliripotiwa kuuawa.

Mvutano huo unaripotiwa katika eneo lililoko kwenye mlima unaopatikana tarafa ya Ngo-Ketunjia, mashariki mwa mji wa Bamenda, kati ya maeneo ya Sagba na Bamessing.

Ripoti za video zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na wanaharakati wanaotaka kujitenga na kuthibitishwa wakazi wa eneo hilo, zilionyesha magari mawili ya kivita yakiwa yamevikanyaga vilipuzi, kabla ya kushambuliwa na kundi la wanamgambo kutoka maeneo hayo, waliojihami kwa zana nzito za kijeshi.

Hilo linakuwa ni shambulio la pili katika wiki mbili. Baadhi ya video hizi zilionyesha miili ya wanajeshi waliouawa ambao wanatoka kikosi cha Uingiliaji wa Haraka (BIR), kitengo cha jeshi maalumu cha Cameroon.

Siyo jeshi wala mamlaka za serikali za eneo hilo waliotoa tamko kuhusu suala hilo na shambulio la aina hiyo liliripotiwa tena wiki iliyopita na mapigano mengine kuzuka katika ukanda huu na kusababisha vifo vya wanajeshi 15 wa serikali.

Mwisho mwa mwezi uliopita Askofu Julius Agbortoko, Naibu wa Kiongozi Mkuu wa Dayosisi ya Mamfé, alitekwa nyara na watu wenye silaha eneo la Manyu, katika mkoa unaozungumza Kiingereza unaokumbwa na mzozo wa makundi ya raia wanaotaka kujitenga.

Katika tukio hilo Askofu Julius Agbortoko alirejea mji jirani wa Kokobuma, ambapo alikuwa amehudhuria hafla ya uzinduzi , vijana wenye silaha waliingia katika chuo cha kiseminari na kujitambulisha kama "wapiganaji wanaotaka kujitenga kwa jimbo lao" na kumteka nyara Askofu Agbortoko badala ya askofu mkuu.

Kwa mujibu wa dayosisi ya Mamfé, watekaji nyara walidai fidia ya faranga milioni 20. Tangu mwanzo wa mzozo wa makundi ya watu wanaotaka kujitenga, waasi wameanzisha mbinu mpya ya utekaji nyara, ambapo wanataka fidia kabla ya kuwachilia mateka. Viongozi wa dini ndiyo hasa wanalengwa na visa hivyo.

**RFI**

# Abdelaziz Bouteflika wa Algeria afariki dunia

**Algiers, ALGERIA**

RAIS wa zamani wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika (84), amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Bouteflika aliongoza nchi hiyo kwa karibu miongo miwili na kuachia madaraka mwaka 2019 baada ya jaribio lake la kugombea muhula wa tano kusababisha maandamano makubwa.

Alikuwa kiungo muhimu katika vita vya kupigania uhuru wa Algeria miaka ya 1950 na 60, ilipofika mwaka 1999, baada ya Algeria kujikwamua kutoka kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilisababisha vifo vya karibu watu 200,000, aliombwa na jeshi la nchi hiyo kupumzika.

Bouteflika hajaonekana hadharani tangu mwaka 2013, baada ya kuugua kiharusi ambacho kiliathiri uwezo wake wa kuzungumza na kutembea.

Kazi yake ya kisiasa ilianza mapema, baada ya uhuru wa Algeria kutoka kwa Ufaransa mwaka 1962, alikuwa naibu waziri wa mambo ya kigeni , rekodi ambayo haijavunjwa hadi wa leo.



Rais Abdelaziz Bouteflik, wakati wa uhai wake.

Alishikilia nafasi hiyo kwa miaka 16 na alikua mwanachama mahiri wa Umoja wa Mataifa, akiwa Rais wa Bunge Umoja wa Mataifa mwaka 1974, alimwalika kiongozi wa Palestina wakati huo Yasser Arafat, kuhutubia taasisi hiyo ya uongozi ya Umoja wa Mataifa katika hatua ambayo haikutarajiwa na iliyotoa mwelekeo katika siasa za mashariki ya kati.

Pia alisisitiza kuwa China inastahili kuwa na uwakilishi katika Umoja wa Mataifa, na kupinga ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini.Kiongozi huyo, anasifika kwa kumpatia Rais wa kwanza wa Afrika ya Kusini huru, Nelson Mandela aliyekuwa kijana mdogo mafunzo yake ya kwanza ya kijeshi.

Bouteflika aliishi uhamishoni miaka ya 1980, kuepuka mashtaka ya ufisadi dhidi yake ambayo hata hivyo yalifutwa.

Alirejea nyumbani miaka ya 1990 na kuchukua hatamu ya uongozi mwaka 1999 - kama kiongozi wa kwanza wa kiraia wa Algeria ndani ya zaidi ya miongo mitatu.

Rais huyo aliyejulikana kama "Boutef" alifanikiwa kuongoza mchakato wa amani kati ya jeshi na wanamgambo waliojihami ambao walikuwa wakipigana katika vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo.

Mwaka 2008, alianzisha mchakato wa kubadilisha katiba ya Algeria ambao uliondoa ukomo wa mihula miwili wa marais na kuchaguliwa tena mara mbili licha ya kukabiliwa na mashtaka ya udanganyifu.

Wakati wa maandamano ya kupigania mageuzi ya uongozi katika nchi za Kiarabu yalipozuka mwaka 2011 kaskazini mwa Afrika, Bouteflika aliongeza haraka ruzuku ya umma na kumaliza hali ya hatari nchini Algeria iliyodumu kwa muda mrefu.

Mara ya mwisho alionekana hadharani mwaka 2017, miaka minne baada ya kupata kiharusi, wakati alipozindua kituo cha metro na msikiti mpya wa Ketchaoua uliokarabatiwa huko Algiers.

Ni katika hafla hiyo ambapo ilitangazwa kwamba rais huyo aliyekuwa akiugua atagombea muhula wa tano mwaka 2019, maandamano yalizuka kupinga hatua hiyo, yakisambaa nchi nzima na yakifanyika kila wiki, hali ambayo haijawahi kushuhudiwa tena.

Baada ya awali kuapa kuahirisha uchaguzi na kuondoka madarakani ndani ya mwaka mmoja, Bouteflika alilazimishwa kujiuzulu na ikiwa ndiyo mara ya mwisho Waalgeria kumuona kiongozi wao aliiyewaongoza kwa miaka 20.

**BBC**



Wanajeshi wa kikosi cha BIR walivamiwa kaskazini magharibi mwa Cameroon. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Conde atajwa kuendelea vizuri baada ya mapinduzi

**AFRIKA MAGHARIBI**

JUMUIYA ya Mataifa ya Ushirikiano wa Kiuchumi ya Afrika Magharibi ( ECOWAS ) imetangaza kuwa rais wa Guinea aliyepinduliwa, Alpha Conde, ambaye amewekwa kizuizini tangu mapinduzi dhidi yake mapema mwezi huu anaendelea vyema.

Katika tangazo lake hilo ECOWAS ilisema ujumbe wake ulotumwa Guinea , umefanikiwa kumuona Conde Ijumaa wiki hii mjini Conakry, akiwa katika kizuizi cha nyumbani katika hoteli moja ya kifahari na kwamba yuko salama.

Hiyo ni taarifa ya kwanza huru kuhusu hali ya rais Conde, tangu kupinduliwa kwake Septemba 5, mwaka huu na jeshi la nchi hiyo na kiongozi wa kijeshi Kanali Hamady Doumbouya, kutangaza kuwa ndiye anayeliongoza taifa hilo.

Ujumbe wa ECOWAS ambao unawajumuisha Rais wa Ghana Nana Akufo Addo, Rais wa Ivory Coast Alassane Outtara, vilevile wamekutana na kiongozi wa kijeshi, Hamady au Mamady Doumbouya.

Taarifa hiyo ilisema mazungumzo yao yalikuwa ya wazi na kirafiki, na kwamba wana imani ya kupatikana suluhisho. Lakini siku moja kabla, ECOWAS ilitangaza marufuku ya kusafiri, vikwazo vya kibiashara dhidi ya walioongoza mapinduzi na familia zao pamoja na kutoa miezi sita ya taifa hilo kufanikisha uchaguzi wa kiraia.

Conde alipinduliwa na jeshi akiwa madarakani baada ya kuzidi kuchukiwa kufuatia kukataa kuondoka ikulu, akiwa amebadilisha katiba ili kuendelea kubaki madarakani.

**DW**

MAKALA

# BARUA YA WAZI KWA WAZIRI WA ELIMU



Na Magabilo Masambu

**Lakini kwa mujibu wa tovuti kuu ya serikali, imeelezwa kwamba sekta ya kilimo ndiyo msingi wa uchumi wa Tanzania. Inachukua karibu nusu ya mapato ya taifa, robo tatu ya mauzo ya bidhaa za nje zinatokana na kilimo ni chanzo cha chakula, pamoja na utoaji wa fursa za ajira kwa karibu asilimia 75 ya Watanzania.**

NDUGU Waziri Prof.Joyce Ndalichako (MB). Salaam!

Kwanza nitumie nafasi hii kukupongeza kwa kuendelea kuaminiwa katika wizara hii kwani umekuwapo katika awamu yote ya tano ya uongozi wa Hayati Rais John Pombe Joseph Magufuli na sasa awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Natambua kwamba Watanzania kwa sasa tuko zaidi ya milioni 60. Katika hali ya kawaida ni jambo la bahati sana kwa idadi hii yote ya Watanzania kupata nafasi ya kuhudumu kama Waziri wa Elimu.

Sina shaka na utendaji wako kwa uzoefu na elimu yako katika sekta ya elimu.

Ndugu Waziri, naandika barua hii kwako kuhusu somo la kilimo katika shule za sekondari. Hali inatisha sana, sina hakika kama wizara mmeliona hili kwa faida ya Tanzania ya sasa, kesho na ijayo. Hali hiyo ni juu ya somo hili la kilimo kuwapo kwa uchache sana katika shule za serikali.

Mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, zaidi ya shule 30 za serikali somo la kilimo linafundishwa katika shule zisizozidi tatu na pengine mwaka huu wa 2021 shule inayotegemewa kufanya mtihani wa taifa wa Kidato cha Nne wa somo la Kilimo ni moja, shule ya sekondari Oldadai.

Lakini kwa mujibu wa tovuti kuu ya serikali, imeelezwa kwamba sekta ya kilimo ndiyo msingi wa uchumi wa Tanzania.

Inachukua karibu nusu ya mapato ya taifa, robo tatu ya mauzo ya bidhaa za nje zinatokana na kilimo ni chanzo cha chakula, pamoja na utoaji wa fursa za ajira kwa karibu asilimia 75 ya Watanzania.

Sasa katika nchi ambayo uchumi wake unategemea kilimo kiasi hiki, inaingiaje akilini somo la kilimo lisiwe somo la lazima kila shule? Taifa lenye njaa litawezaje kujitegemea? Ni ukweli kwamba misingi tuliyo nayo kwa sasa katika sekta ya kilimo inatokana na mipango ya awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika jitihada za kuwafanya Watanzania wajitegemee chini ya sera ya ujamaa ambayo msingi wake mkuu ulikuwa ni kilimo na ufundi.

Nimesoma pia hotuba yako Ndugu Waziri juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2021/22 ukurasa wa 16 kuhusu uendelezaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Umeeleza juhudi zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchuliwa katika eneo hilo na mafunzo ya ufundi.

Maana yake ni maandalizi ya kuwa na viwanda kwa kuwa wataalam tutakuwa nao lakini ni muhimu kufahamu kuwa hatuwezi kuwa na viwanda bila malighafi safi kutoka mashambani. Pia sjaona mahali popote katika hotuba ambako kuna mpango kabambe wa kuajiri walimu wengi wa kilimo maana shule zipo ni suala la walimu tu hatuwezi kusema labda kunahitajika kujengwa shule mpya za kilimo.

Nakubali kwamba kwenye eneo la kuboresha shule za ufundi serikali ya awamu ya tano imefanya vizuri sana na wewe ukiwa waziri ukahakikisha usimamizi wa maboresho hayo ukafanyika kwa viwango.

Binafsi nilisoma shule ya ufundi Ifunda kwa hiyo nafahamu hali ilivyokuwa wakati wetu. Shule zilichakaa sana ni kama wakati fulani zilisahulika ilikuwa ni hali ya kawaida mvua iliponyesha usiku kuamka na kujibanza sehemu ambazo maji hayakuvuji, leo karibu shule zote unaweza kudhani ni vyuo vikuu hongera sana kwa usimamizi.

Nguvu ile ile ihamie sasa kwenye kuajiri walimu wa kilimo na faida yake kubwa ni kwamba kila mtu akihitimu akiwa anafahamu sawasawa somo la kilimo maana yake serikali itatumia gharama kidogo sana katika kuajiri maofisa kilimo na pengine kutofanya hivyo siku za mbeleni.

Kila mtu atakuwa na uelewa kuhusu namna bora ya kuzalisha mazao mazuri kwa wingi jambo ambalo litapunguza umasikini wa watu na kuongeza ajira binafsi kwenye sekta ya kilimo kama tulivyoona kwamba kwa sasa zaidi ya asilimia 75 wanajiajiri huko.

Kama kweli utafiti umefanyika vya kutosha na kutoa matokeo kwamba msingi wa uchumi wa nchi hii unategemea kilimo, hakuna namna nyingine yoyote itakayoondoa umasikini wa Watanzania isipokuwa kilimo. Hata hivyo, kilimo bila walimu ni sawa na saa bila betri! Naamini wapo wahitimu wanaotoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na vyuo vingine vya kilimo ambao kwa uchache wao wangelitumika kufundisha na kuzalisha walimu wengi kwa baadaye.

Mwisho, ni kweli kwamba tuko katika soko huria la uchumi duniani lakini tusijisahau tukaendelea kuwa wateja wa bidhaa za dunia tukashindwa kutengeneza wateja wetu kutokana na bidhaa tunazozalisha hapa kwetu hasa kutoka mashambani kutokuwa na shule za kilimo ni kulizika taifa na viwanda bila kilimo, ni sawa na jembe bila mpini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Bathazal alivyoziimarisha, kuzivunja bendi



Na Adam Fungamwango

**Mashabiki wengi wa muziki, hawajui kuwa Abel ndiye aliyeibomoa Sikinde 1982 kwa kuwachukua kina Joseph Mulenga, Abdallah Gama, Shaaban Dede na Suleiman Mwanyiro kuwapeleka Bima Lee.**

UKIZUNGUMZIA historia ya ustawi wa muziki Tanzania, huwezi kukosa kulifikiria au kulitaja jila la Abel Bathazal. Sidhani kama kuna mwanamuziki wa kuanzia miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990 akakosa kumfahamu mwanamuziki huyo ambaye alifariki dunia katikati ya miaka ya 1990.

Jila lake halisi lilikuwa Abel Barthazal Mgaitembo. Alikuwa mmoja wa wapiga solo mahiri waliowahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania. Ndiye aliyepiga nyimbo nyingi za Nuta Jazz 'Msondo Ngoma' na baadaye Juwata Jazz Band kuanzia miaka ya 1970, hadi 1977, alipojiengua na kwenda kuunda bendi ya Dar International na kumwachia solo, Said Mabera (naye sasa ni marehemu).

Achana na umahiri wake wa kupiga gitaa la solo. Bathazal anajulikana na wanamuziki na wamiliki wa bendi kuwa ni mmoja wa watu wanaoweza kuunda bendi, kuiimarisha, lakini pia kuidhoofisha au kuiua kabisa.

Kutokana na umahiri wake huo, akapachikwa jina la 'Bwana Mipango'. Ukiwa una vyombo vyako unataka wanamuziki, ukimwona Bathazal basi ujue utawapata wanamuziki hata wenye majina makubwa kiurahisi zaidi.

Alikuwa na uwezo mkubwa wa ushawishi kwa mwanamuziki yoyote yule hata awe mgumu vipi. Waswahili wanasema hakuna mkate mgumu mbele ya chai.

Kwa upande wa pili alikuwa anaogopwa kama ukoma. Aliogopwa na wamiliki na viongozi wa bendi. Siku akija kwenye bendi yenu, basi mkae mkijua baada ya siku mbili au tatu, mtalia kilio cha mbwa.

Ni lazima atakuwa amekuja kuwarubuni wanamuziki tegemezi kuondoka.

Huyu ndiye Abel Bathazal kwa upande wake wa pili wa shilingi, ukiacha kuwa ni mwanamuziki mpiga gita la solo mahiri.

Alitokea Muheza Tanga, akaja Dar es Salaam kwenye bendi ya Western Jazz, lakini kwa kuhofu watanyang'anywa walimpeleka Kilosa Jazz kwa muda wakati wanajipanga ili wamrudishe. Inasemekana Kilosa Jazz wakagoma kumrudisha. Wakamtaifisha.

Nuta Jazz nao wakaenda kufanya umafia na kumchukua. Hapo ndipo kila shabiki wa muziki alishuhudia Balaa Lake.

Mwaka 1977, wakati huo bendi inabadilisha jina kutoka Nuta kwenda Juwata Jazz, alijiengua na kwenda kuunda bendi ya Dar Intenational. Ilikuwa kidogo amchukue na Muhidini Gurumo kutoka Msondo, lakini ikashindikana.

Siku zote mzuri wako ndiye mbaya wako. Mmiliki wa Dar International alipata pigo, baada ya Abel kuwachukua wanamuziki karibu wote wa bendi hiyo na kuwapeleka kwenye bendi nyingine mpya, iitwayo Mlimani Park Orchestra.

Mipango ilikuwa ikifanywa kimya kimya kati ya Barthazal na wamiliki wa chama cha madereva Taxi Tanzania. Ikabidi sasa mmiliki wa Dar International kumrudisha Marijani Rajab aliyesimamishwa baada ya kugombana na Barthazal.

Abel akaenda Msondo sasa kumchukua Gurumo ambaye mwanzo ilishindikana kwenda Dar International mwaka 1978.

Baadaye tena mwaka 1979 akawachukua Msondo Hassan Bitchuka, Selemani Mwanyiro, Juma Town na kuwaleta Sikinde.

Mashabiki wengi wa muziki, hawajui kuwa Abel ndiye aliyeibomoa Sikinde 1982 kwa kuwachukua kina Joseph Mulenga, Abdallah Gama, Shaaban Dede na Suleiman Mwanyiro kuwapeleka Bima Lee. Wengi hawajui kuwa alijiunga na bendi hiyo na kuitengeneza vizuri, lakini yeye mwenyewe hakukaa sana na wala hakurekodi.

Hata Bitchuka alikuwa ende Bima Lee lakini ilishindikana.

Abel akaenda Orchestra Safari Sound (OSS) chini ya Ndala Kasheba. Alipoondoka Kasheba, alifanya unyama kwa kwenda Sikinde mwaka 1985 kuwachukua Bitchuka, Gurumo, Kassim Rashid, John Ngosha, Ally Makunguru na kuiimarisha OSS ambayo sasa ikawa na mtindo wa Ndekule badala ya Dukuduku.

Mwaka 1987 Bitchuka alirejea Sikinde na kwa hasira, Barthazl akaenda kukomba wanamuziki sita Sikinde, wakiwamo Max Bushoke, Cosmas Chidumule, Hamisi Juma na wengineo kuwapeleka Ndekule.

Kama vile haitoshi, mwaka 1990, Jeshi la Magereza kwa kuona umuhimu wake, nalo lilimwita kwenye bendi hiyo si kwa ajili ya kupiga tu, bali hata kuiimarisha bendi. Ndipo alipowachukua kina Nana Njige, Hassan Kunyata na kuwachukua mpaka baadhi ya wanamuziki wa Kikongomani OSS kuwapeleka Magereza Jazz.

Kama kawaida kila anapokwenda au kusaidia kuunda bendi ni lazima itatisha tu. Hapo ndipo Magereza ikaja na mtindo wa 'Mkote Ngoma' na ikitamba kwa vibao ambavyo yeye mwenyewe alipiga solo kama vile 'Ashura', 'Pilipili', 'Edina', na 'Akumulikaye Mchana'.

**Kwa maoni piga 0716 350534**

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana?


Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa.

Donald. Kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi- 24

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




SASA alijiona mwepesi. Alijua kila kitu. Lakini kazi yote alitaka kuwakabidhi polisi, bila kutambua kama yeye anajua kitu. Alichofanya ni kuwasaidia ushahidi ili kuwarahisishia kazi. Na kilichomkasirisha zaidi ni kuonekana anasakwa, labda kwa ajili ya kuficha ushahidi. Yupo mtu anayeonekana anataka kuzima ushahidi huo wa mauaji kwa sababu yeye anajua kila kitu, ila tu anauficha kutokana baadhi ya wahusika ni wazazi wake.

"Sawa Donald, hii simu naichukua. Na nakuhakikishia wiki hii tunaweza kumaliza utata wote. Tunaweza kujua ni nani au kila nani wanahusika na ikiwezekana kuwatia mbaroni."

"Ahsante sana afande. Mimi nipo kwa msaada utakaohitajika."

Kwa hili alilofanya, tayari Donald alijiona kama hata kama wahusika wakikamatwa, yeye hatoweza kuwa hatiani. Ni kwa sababu ametoa ushahidi na ushirikiano. Hii ni tofauti na awali alipoitwa kwenye Makao Makuu ya Polisi. Aliona hata kama akitoa ushahidi huo hawatomuamini na wangeweza kumuweka ndani kwa kumshuku kuwa huenda na yeye anahusika kwa njia moja ama nyingine.

******************************

Kilikuwa ni kakao kizito. Kilimhusisha Inspekta Andrew mwenyewe. Koplo Peter alikuwapo. Kulikuwa na mtaalam wa teknolojia ya Tehama kutoka Makao Makuu ya Polisi. Afisa mmoja kutoka Mamlaka ya Mawasiliano, pamoja na mtaalam mmoja kutoka huko.

Baada ya mazungumzo ya muda mrefu, pamoja na kuwahakikishia na kuwapa namba zote zilizoonyesha meseji zile awali zilitoka kwenye namba gani na kuzikapekewa tena kwenye namba zingine, watu wa Mamlaka ya Mawasiliano wakawa wamemaliza kazi yao.

Kazi hiyo ilifanywa kwa kibali maalum. Baada ya kumaliza, Afisa na mtaalam wa Tehama wa Mamlaka ya Mawasiliano wakawa wamemaliza kazi yao. Wakaagana na maafisa wa polisi na kuwaacha sasa wafanye kazi iliyokusudiwa.

Waliitwa maafisa wengine wawili wa polisi kwa ajili ya kuzifanyia tathmini meseji ambazo tayari zlikuwa zimeshaonyesha zimetoka wapi na kwenda wapi.

"Samahani mpenzi, nimepoteza simu yangu muda si mrefu, ndiyo maana nimetumia namba ambayo ni ngeni nimeomba kwa rafiki yangu, nakuomba uje hapa Afrika Sana, niko hapa nakusubiri."

Meseji hii kwa mujibu wa wataalam wa IT ni kwamba asili yake ilianza kwenye namba inayomilikiwa na Peterson Donald.

Hii iliwashangaza kidogo maafande. "Kwa nini meseji imeandika na mtu aliyesajiliwa kwa jina la Peterson Donald, wakati aliyekwenda kuuawa ni mpenzi wa Donald?" Alihoji mmoja wa maafande waliokuwapo kikaoni.

"Kumbuka kuwa mpenzi wa marehemu Tausi anaitwa Donald Peterson." Alidakia Koplo Peter.

"Inawezekana muuaji ni huyu huyu Donald, alisajili namba ya simu kwa kuligeuza jina akianzia na jina la baba yake. Ndiye aliyemuandikia mpenzi wake aende Afrika Sana, akafanya tukio hili kwa sababu labda ya wivu wa kimapenzi." Afande mwingine alichangia.

"Mimi nadhani tusiwe na haraka sana. Hebu fanya kama unataka kumtumia pesa kwenye namba yake, halafu litatoka jina gani." Inspekta Andrew alimwambia Koplo Peter. Akafanya kama alivyoambiwa.

"Jina ni Donald Peterson." Aliwaambia wenzake.

"Sasa Donald Peterson ndiyo Peterson Donald?" Akauliza Inspekta Andrew.

"Afande kumbuka kuwa hizo ni namba mbili tofauti. Hii aliyotumiwa meseji marehemu Tausi ni nyingine na anayotumia sasa Donald ni nyingine, hivyo ile inaweza alisajili kwa kuanzia jina la baba yake, na hii anayotumua akaanza na la kwake." Afisa wa Polisi wa kwanza alidakia.

"Kwa maana hiyo Donald ndiye muuaji wa mpenzi wake Tausi?" Koplo Peter akahoji.

"Chochote kinawezakana, ila hebu tujiulize hivi Donald hana baba?" Ilikuwa ni sauti ya Inspekta Andrew.

Ingawa ushahidi kama unataka kuelekea kumbana Donald, lakini bado Inspekta Andrew akili yake haikuamini kuwa kijana huyo anaweza kufanya hivyo. Mwanzoni alidhani hivyo. Lakini alipokutana naye. Mazungumzo yake na ushirikiano alioutoa mpaka kumwambia akatafute simu kwenye mabaki ya gari, alijua kuna kitu kikubwa zaidi kuliko ambacho askari wenzake wanataka kuamini.

"Hebu twendeni hiyo ya pili." Aliamuru Inspekta.

"Mpenzi nimemtuma kijana mmoja wa bodaboda aje kukuchukua. Ni rafiki yangu na huwa namlipa kwa mwezi kwa mambo ya dharura. Nimekuita ghafla ndiyo maana sitaki uingie gharama, atakuleta salama hadi huku."

Meseji hii ya pili haikuwa na mjadala mzito sana kwa sababu haikuwa na kipya, ilitoka kwa mtu mwenye namba ile ile, kilichobadilika ni kwamba aliyetakiwa kwenda Sinza alikodiwa bodaboda. Na hii iliwafanya maafande hao waamini kuwa aliyetuma meseji hiyo alikuwa na nia ya dhati ya kumuua, kwani hakutaka kusingizio chochote kutoka kwenye windo lake.

> **"Afande kumbuka kuwa hizo ni namba mbili tofauti. Hii aliyotumiwa meseji marehemu Tausi ni nyingine na anayotumia sasa Donald ni nyingine, hivyo ile inaweza alisajili kwa kuanzia jina la baba yake, na hii anayotumua akaanza na la kwake." Afisa wa Polisi wa kwanza alidakia.**

Maafande wote walijua kuwa marehemu alikubali kwenda kule akidhania anaitwa na mpenzi wake Donald, ambaye alipoteza simu yake ya mkononi na anatumia namba ya mtu mwingine ambaye ni rafiki yake aliyenaye hapo.

"Baba, amevaa sketi fupi yenye mistari myeupe na myeusi na blauzi nyeupe." Meseji ya tatu iliwekwa hadharani kwa ajili ya kujadiliwa. Katika meseji zote, tatu, hii pekee ndiyo iliyotoka kwenye namba tofauti. Namba hii ya simu kwa mujibu wa watu wa IT, inamilikiwa na mwanamke mmoja anaitwa Doroth Masiku. Na ilionekana ikapelekwa kwenye namba ya simu ya Peterson Donald.

Meseji ya nne iliyosomeka "Amevaa sketi fupi yenye mistari myeupe na myeusi kama ya pundamilia hivi na blauzi nyeupe." Hii ilitoka kwenye namba ile ile ya Peterson Peter, lakini nayo ikapelekwa kwenye namba ya simu iliyosajiliwa kwa jina la Ben Bogota.

"Inavyoonekana meseji ya tatu iliyoka kwa mwanamama, ikapelekwa kwa Peterson, halafu jamaa akaipeleka kwa Bogota. Hapa inaonyesha kulikuwa na mawasiliano ya watu tofauti kwa ajili ya kuhakikisha marehemu anakwenda eneo husika, hawampotezi, na hawa ndiyo wauaji kwenyewe wa marehemu Tausi." Alisema afisa mmoja wa polisi akiwa na hasira.

"Hilo neno baba, linanifanya nimtoe Donald kwenye kundi la wauaji. Sidhani kama kuna mwanamke, au msichana ambaye yuko kwenye kundi la wauaji kwa umri wake anaweza kumwita kijana kama yule baba." Inspekta Andrew alidakia. Wenzake walinyamaza. Wengine wakatikisa kichwa kukubaliana na hilo. "Nadhani tufanye kitu kimoja tu, tuwapigie Mamlaka ya Mawasiliano watupe umri sahihi wa Peterson Donald kitu ambacho tulisahau." Koplo Andrew alishauri.

Alipokubaliwa aliondoka. Dakika moja baadaye alirejea kikaoni. "Miaka yake ni 65." Aliwaambia wenzake.

"Sasa ni hivi. Kama baba yake mzazi Donald yuko hai, nadhani tuanze naye. Tumfuatilie. Nadhani kama yupo, ni kuichukua tu simu yake, inaweza kutupa kila kitu." Yalikuwa ni maneno ya Inspekta Andrew."

"Ina maana baba anaweza kumuua mkwewe kweli?" Afande mmoja akahoji.

"Nishawahi kusikia hadithi moja ya kijana anataka kumuoa msichana fulani, lakini msichana huyo akauawa na baba wa kijana huyo kwa sababu ya wivu wa kimapenzi. Kumbe alikuwa ni mchepuko wake. Dunia ina mambo hii. Usiione hivi." Maafisa hao wa polisi wakamaliza kikao chao.

**ITAENDELEA JUMAPILI**









# HARMONIZE APELEKA JOTO 'ARIZONA'

STAA wa Bongo Fleva, Harmonize, amewasha kibiriti karibu na nyasi, baada ya tangazo lake la kutoa albam yake ya tatu, kuibua maoni tofauti kwa mashabiki wake.

Harmonize anaendelea na ziara yake nchini Marekani, na akiwa huko ametangaza ujio wa Albam hiyo aliyoita 'Arizona' ambayo inaandaliwa na mtayarishaji wa muziki Mr Simon kutoka nchini Norway.

Baadhi ya mashabiki wake wamempongeza kwa kupiga hatua hiyo, wakisema ni jambo zuri kufanya kazi na mtayarishaji wa muziki mkubwa.



# Wakazi ataka mjadala kukatwa asilimia 30

RAPA mkali nchini Wakazi, amesema kitendo cha serikali kukata asilimia 30 ya pesa zinazotokana na mrabaha wa kazi za wasanii, ni jambo linalohitaji mjadala wa kina.

Amesema COSOTA ambacho ni chombo cha serikali kinachosimamia hatimiliki kinahitaji kuendelea kwa kupata mapato ya ndani, lakini kuchukua kiasi hicho kunaleta ukakasi katika midomo ya wasanii.

"Kumbuka sisi kama wasanii muziki wetu unasambazwa kupitia mitandao mbalimbali ambayo nayo inakata, kuanzia asilimia 25 hadi 50. Si watu wa kwanza kuchukua pesa zinazotokana na kazi zetu, lakini kama chombo cha serikali inatakiwa kuchukua baada ya kuwapo kwa mjadala," amesema.

LIVE IN PLAY

BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP

CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA




MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 19 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4518 | GO Ahead Eagles vs PEC Zwolle | 2.39 | 3.26 | 2.86 |
| 13:30 | 5534 | Empoli vs Sampdoria | 2.58 | 3.59 | 2.58 |
| 13:30 | 5555 | Giresunspor vs Konyaspor | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 14:00 | 3523 | Nice vs Monaco | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 14:00 | 4247 | Dundee Utd vs Dundee FC | 2.52 | 3.11 | 2.81 |
| 14:30 | 3778 | St Truiden vs Racing Genk | 3.74 | 3.74 | 1.85 |
| 15:00 | 2307 | Randers vs Nordsjalland | 2.26 | 3.55 | 2.86 |
| 15:00 | 4888 | Mallorca vs Villarreal | 3.51 | 3.11 | 2.23 |
| 16:00 | 1200 | Venezia vs Spezia | 2.41 | 3.46 | 2.86 |
| 16:00 | 2891 | Clermont Foot vs Brest | 1.85 | 3.73 | 3.88 |
| 16:00 | 3057 | Reims vs Lorient | 2.18 | 3.32 | 3.27 |
| 16:00 | 3238 | West Ham vs Manchester Utd | 4.14 | 3.75 | 1.83 |
| 16:00 | 3504 | Angers vs Nantes | 2.08 | 3.28 | 3.57 |
| 16:00 | 4070 | Troyes vs Montpellier | 2.49 | 3.43 | 2.69 |
| 16:00 | 4317 | Galatasaray vs Alanyaspor | 1.52 | 4.35 | 5.33 |
| 16:00 | 4538 | Moroka Swallows FC vs SuperSport Utd | 2.81 | 2.71 | 2.81 |
| 16:00 | 5535 | Brighton vs Leicester | 2.68 | 3.18 | 2.73 |
| 16:30 | 1694 | Stuttgart vs Bayer Leverkusen | 3.08 | 3.62 | 2.15 |
| 16:30 | 3516 | Nizhny Novgorod vs Arsenal Tula | 2.36 | 3.05 | 3.10 |
| 17:00 | 1170 | Sparta Prague vs Baumit Jablonec | 1.39 | 5.01 | 7.02 |
| 17:00 | 1405 | Royal Antwerp vs RFC Seraing | 1.51 | 4.44 | 5.33 |
| 17:00 | 2699 | Livingston vs Celtic | 5.73 | 4.35 | 1.49 |
| 17:00 | 2843 | Sonderjyske vs Brondby | 3.30 | 3.50 | 2.06 |
| 17:00 | 3220 | Rangers vs Motherwell | 1.27 | 5.33 | 9.86 |
| 17:15 | 3797 | Real Sociedad vs Sevilla FC | 2.60 | 3.14 | 2.84 |
| 17:30 | 4576 | FC Vizela vs Pacos Ferreira | 2.40 | 3.11 | 2.96 |
| 17:45 | 3463 | Heracles Almelo vs AZ Alkmaar | 3.94 | 3.70 | 1.81 |
| 17:45 | 4064 | Vitesse Arnhem vs Twente | 1.97 | 3.55 | 3.50 |
| 18:00 | 2248 | Mamelodi Sundowns vs TS Galaxy FC | 1.41 | 4.21 | 7.45 |
| 18:00 | 3351 | Marseille vs Rennes | 1.94 | 3.43 | 3.88 |
| 18:00 | 3662 | RB Salzburg vs Rapid Vienna | 1.28 | 5.43 | 7.75 |
| 18:30 | 2774 | Borussia Dortmund vs Union Berlin | 1.35 | 5.37 | 7.16 |
| 18:30 | 3455 | Tottenham vs Chelsea | 4.62 | 3.67 | 1.77 |
| 19:00 | 1054 | Sarpsborg vs Rosenborg | 3.05 | 3.34 | 2.23 |
| 19:00 | 1245 | Valerenga vs Molde | 2.57 | 3.81 | 2.36 |
| 19:00 | 2362 | Basaksehir vs Fenerbahce | 3.45 | 3.41 | 2.03 |
| 19:00 | 3751 | Hatayspor vs Kayserispor | 1.90 | 3.70 | 3.60 |
| 19:00 | 4049 | Verona vs Roma | 3.93 | 3.83 | 1.85 |
| 19:00 | 4618 | Sochi vs Dinamo Moscow | 2.60 | 3.14 | 2.70 |
| 19:00 | 5040 | Lazio vs Cagliari | 1.48 | 4.72 | 6.03 |
| 19:00 | 5852 | Copenhagen vs Midtjylland | 1.91 | 3.65 | 3.60 |
| 19:30 | 1482 | Betis vs Espanyol | 2.00 | 3.31 | 3.96 |
| 19:30 | 5624 | Standard Liege vs Anderlecht | 3.06 | 3.55 | 2.14 |
| 20:00 | 2254 | Porto vs Moreirense | 1.21 | 6.10 | 11.81 |
| 20:30 | 2274 | Lamia vs Olympiakos | 11.86 | 5.73 | 1.23 |
| 20:30 | 2647 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 1.81 | 3.77 | 4.07 |
| 21:45 | 3632 | Paris St Germain vs Lyon | 1.41 | 5.01 | 6.50 |
| 21:45 | 4270 | Juventus vs AC Milan | 2.21 | 3.42 | 3.22 |
| 22:00 | 5773 | Valencia vs Real Madrid | 3.59 | 3.63 | 2.00 |
| 22:30 | 2991 | GD Estoril vs Sporting Lisbon | 5.71 | 3.84 | 1.56 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ARTETA HANA UHAKIKA NA LENO



**LONDON,** England

MIKEL Arteta hana uhakika kama Bernd Leno atakuwa golikipa chaguo la kwanza katika kikosi chake msimu huu.


Hatima ya Leno bado haijafahamika pale Arsenal tangu ujio wa Aaron Ramsdale, ambaye ni chaguo la kwanza kwa sasa.

Kipa huyo aliachwa na Arteta kwenye mechi ya Ligi Kuu England wakati Arsenal ilipopata ushindi wa kwanza wa bao 1-0 msimu huu dhidi ya Norwich City.

"Siwezi kumpa ahadi Leno kuhusu uhakika wa namba, muhimu kupambana na kucheza kwa bidii, haiwezi kujitokeza kirahisi," alisema Arteta akinukuliwa na Sky Sport.

"Kwa sasa ni jambo gumu kusema yeye anaweza kucheza mara kwa mara kwa sababu hiyo itategemea na kiwango chake uwanjani. "Hivyo siwezi kusema anaweza kuwa chaguo namba moja kwa sasa, ngoja tusubiri tuone nini kitajiri kwa kikosi chetu kwa sababu msimu ndio kwanza umeanza.

Leno alianza vibaya msimu akiruhusu mabao mengi katika mechi tatu alizopangwa na Arteta anaona nafasi yake ni ndogo kuwapo katika kikosi cha kwanza.



# *Raiola achochea Pogba kurudi Juventus*

**MANCHESTER,** England

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola, amebainisha nyota huyo ana nafasi kubwa ya kurejea Juventus.

Pogba kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Manchester United, huku pia klabu nyingine zikitajwa kuwania huduma yake.

Lakini Raiola anaona bado kuna uwezekano mkubwa kwa Pogba kutua Juventus mwishoni mwa msimu huu.


Pogba anamaliza mkataba wake na Manchester United mwishoni mwa msimu huu na bado kuna sitofahamu kuhusu yeye kusaini mkataba mpya.

Bado haijawekwa wazi kama nyota huyu ataendelea kuwao United au ataondoka kama mchezaji huru msimu ujao.

Akizungumza na Corriere dello Sport, Raiola amesema kuna vitu vinaendelea nyuma ya pazia na kuna uwezekano mkubwa wa Pogba kurudi Juventus.

"Mkataba wa Pogba unaisha mwakani, tutakaa na Manchester United halafu tutaona. Ni ukweli Turin bado ipo moyoni mwake na anajali sana haya mambo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL ATABIRI HATIMA YA KANE

●●● Afunguka bado Manchester City wako katika nafasi nzuri ya kumnasa mshambuliaji huyo...

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema bado anafikiria kuna nafasi ya mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, kujiunga na Manchester City hivi karibuni.

Manchester City ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England walikuwa katika hesabu ndefu za kumsajili Kane ila mambo 'yalibuma' baada ya klabu yake kumzuia kuondoka.

**Ilikuwa Mei, mwaka jana nyota huyo alipofunguka anahitaji kupata changamoto mpya na timu ambayo ilikuwa inapewa nafasi ya kumpata ilikuwa ni Manchester City inayonolewa na Pep Guardiola.**

Pia hata Chelsea nao walikuwa wanahitaji huduma ya Kane ambaye alishinda kiatu cha ufungaji bora msimu uliopita, nao walikwama wakaishia kuipata saini ya Romelu Lukaku ambaye alikuwa anakipiga ndani ya Inter Milan huko nchini Italia.

Tuchel alipouliziwa kuhusu 'dili' la Kane alisema:"Nadhani kuna jambo ambalo linaweza kutokea kwa wakati ujao. "Kwetu sisi hatukuwa na mpango wa kufanya hivyo na sijasema kwamba tunahitaji kumnunua mchezaji huyo.

"Ninadhani kuna jambo ambalo lingetokea ikiwa angepata nafasi ya kwenda Manchester City hivyo kuna mambo ambayo yapo."

## ZISIKUPITE

### ADEYEMI ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 19, kutoka klabu ya Red Bull Salzburg. ***(Mundo Deportivo)***

### RUDIGER MAMBO MAGUMU

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger (28), huenda akauzwa ili kufadhili ununuzi wa beki wa Sevilla, Jules Kounde. Mchezaji huyo ambaye ni raia wa Ujerumani ananyatiwa na klabu za PSG na Real Madrid, lakini ameonekana kuwa bado anahitajika na kocha, Thomas Tuchel. ***(Football 365)***

### BARCA ILIMTAKA RODRIGO

BARCELONA ilimtaka mshambuliaji wa Leeds United, Rodrigo mwenye umri wa miaka 30 katika siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho msimu huu, lakini klabu hiyo yake ikakataa ofa iliyotolewa kumuuza Mhispania huyo. ***(The Athletic)***

### MARTINEZ, INTER SAFI

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez ameripotiwa kukaribia kuongeza mkataba mpya na klabu hiyo ya Serie A, ikimaanisha Arsenal na Tottenham watalazimika kutumia kitita kikubwa cha fedha kama wataendelea na nia yao ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Gazzetta dello Sport)***

### WILSHERE AWEKA MGOMO

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Jack Wilshere hataki makubaliano ya kulipwa kwa mechi atakazoshiriki katika Uwanja wa Emirates, baada ya kocha, Mikel Arteta kumruhusu kushiriki mazoezi katika uwanja wa timu hiyo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ameichezea England mara 34 lakini amekosa klabu tangu alipoondoka Bournemouth mapema mwaka huu. ***(Metro)***

### RICE ATAJWA UNITED

MANCHESTER United imemfanya nyota wa West Ham, Declan Rice kuwa kipaumbele chao namba moja kwenye usajili wa majira ya joto yajayo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 anataka kujiunga na Mashetani Wekundu hao. ***(Independent)***

### STERLING KUTUA BARCA

BARCELONA itajaribu kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26 kwa mkopo kutoka Manchester City katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Sport)***

### POGBA NJIA NYEUPE

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola, amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 anaweza kujiunga na Juventus wakati mkataba wake utakapomaliza kule Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Rai Sport via Corriere dello Sport)***

### MESSI KUTUA MAREKANI

STRAIKA wa Inter Miami, Gonzalo Higuain amesema klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Marekani (MLS) zina malengo ya kumsajili mchezaji mwenzake wa Argentina, Lionel Messi wakati mkataba wa mchezaji huyo na klabu ya Paris St-Germain utakapomalizika ifikapo mwaka 2023. ***(ESPN Argentina)***

HABARI MICHEZO

## Kocha Coastal Union mtegoni

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umesema moja ya mikakati yao waliyompa Kocha Mkuu, Melis Medo ni kuhakikisha katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, timu hiyo ya jijini Tanga inamaliza kwenye nafasi nne za juu, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno, aliliambia gazeti hili klabu yao ina malengo makubwa na ndio sababu wameimarisha benchi la ufundi.

Mgweno alisema wana imani watafanya vizuri katika msimu huu mpya kutokana na maboresho yaliyofanyika baada ya kubaini upungufu wao ya msimu uliopita.

"Kwa usajili wetu na maboresho makubwa tuliyofanya kwenye benchi la ufundi tuna matarajio ya kufikia malengo yetu, na Kocha wetu Medo anafahamu hilo, naye tumempatia anachokitaka ili wote twende sambamba," alisema Mgweno.

Aliongeza wanafahamu vyema msimu ujao utakuwa na ushindani kutokana na timu zote kujiimarisha na zawadi za fedha zitakazotolewa baada ya kumalizika kwa ligi.

Coastal Union itafungua msimu mpya kwa kuwakaribisha Azam FC mchezo utakaochezwa Septemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

## Simba Muheza watoa misaada

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIKA kusheherekea Simba Day mashabiki na viongozi wa timu hiyo katika Tawi la Majengo Shimoni lililoko kwenye Wilaya ya Muheza jijini Tanga wametoa misaada mbalimbali kwa watoto wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Mbaramo.

Mashabiki wa tawi hilo walifika katika shule hiyo kwa maandamano kutoka kwenye tawi lao na kupitia Kituo Kikuu cha mabasi Muheza, mtaa wa Amtico, Majani Mapana, Mbaramo mahakamani hadi kuingia kwenye eneo la shule na kukabidhi misaada hiyo huku wakisindikizwa na burudani ya muziki.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu wa Tawi la Majengo Shimoni, Fraternus Siliro, alisema viongozi na mashabiki wa tawi lao waliungana na wenzao wa Kicheba kutoa misaada hiyo kama sehemu ya kuwa karibu na jamii.

Siliro alisema mashabiki hao waliguswa na mazingira wanaoishi watoto hao na kuamua kuchanga fedha ambazo zilisaidia kununua vifaa ambavyo watoto hao walikuwa wanavihitaji.

Alitaja baadhi ya vitu walivyotoa ni vyakula, sabuni, maji na mifuko ya saruji kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa mabweni ya kulala wanafunzi hao ambao ujenzi wake unaendelea.

# GALAXY YAIFUATA SIMBA LIGI YA MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam, itakutana na Jwaneng Galaxy FC ya Botswana katika mechi ya hatua ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kati ya Oktoba 15 na 17, mwaka huu.

**Mechi ya marudiano itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini itachezwa kati ya Oktoba 22 na 24, mwaka huu.**

Jwaneng Galaxy ilikubali kichapo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya DFC 8eme Arrondissement ya Afrika ya Kati katika mchezo wa marudiano hapo juzi, lakini imesonga mbele kutokana na ushindi wa mabao 2-0 iliopata nyumbani walipokutana kwenye mechi ya kwanza.

Timu hiyo inacheza Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya Ligi Kuu Botswana kuvunjwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVICO-19.

Zikiwa zimesalia mechi 10 kwa kila timu kwenye Ligi Kuu Botswana inayoshirikisha timu 16, ndipo Shirikisho la Soka la nchi hiyo ilitangaza kuiteua timu hiyo kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu kwa sababu ilikuwa inaongoza kwenye msimamo wa ligi.

Timu hiyo iliazishwa mwaka 2015 kwa muungano wa klabu mbili za Jwaneng Comets na Debswana Toungsters. Jwaneng Galaxy ilikuwa tayari imecheza mechi 20, ikishinda michezo 12, sare tano na kufungwa michezo mitatu, ikiwa imejikusanyia pointi 41.

Itakuwa ni mara ya tatu kwa Simba kucheza na timu kutoka Botswana katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mara ya kwanza ikiwa na ni mwaka 2003, ambapo ilikutana na BDF na kuitoa kwa jumla ya mabao 4-2 huku msimu wa 2018/19 Wekundu wa Msimbazi iliwaondoa Mbabane Swallows kwa jumla ya mabao 8-1.

Katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, Simba iliondolewa na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini katika hatua ya robo fainali kwa kufungwa jumla ya mabao 4-3.

Hata hivyo, kwa hatua hiyo iliyofika, iliiongezea Tanzania pointi na msimu huu kupata nafasi ya kuwakilishwa na timu nne katika mashindano yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akipiga mpira wakati wa mashindano ya gofu ya kuwania Kombe la Mkuu wa Majeshi (CDF Trophy 2021), yanayofanyika kwenye viwanja vya Lugalo jijini Dar es Salaam. Mdhamini Mkuu wa mashindano hayo yatakayochezwa kwa siku mbili ni Benki ya NMB. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Omog arejea kuiongoza Mtibwa Sugar*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar umethibitisha kufanya mazungumzo na makubaliano ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Joseph Omog kwa ajili ya kukinoa kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema mazungumzo na Omog yamefikia mahali pazuri na Macameroon huyo anatarajiwa kutua nchini leo ili kusaini mkataba na hatimaye kuanza kazi rasmi.

Kifaru alisema walipokea maombi kutoka kwa makocha mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ikiwamo Omog ambaye mabosi wa klabu hiyo waliridhishwa na rekodi yake.

"Omog ni kocha wetu mpya na ataingia nchini Jumapili saa 8:00 ya usiku, tayari kwa ajili ya kuanza kukinoa kikosi cha Mtibwa Sugar, uongozi umeridhishwa na CV zake pia ni sahihi kwetu kwa sababu analifahamu vizuri soka la Tanzania na aina ya wachezaji tuliokuwa nao.

"Kila mdau wa soka anatambua Omog amewahi kufundisha Simba kwa mafanikio makubwa, kwa sababu msimu huu tunajambo kubwa, ndio sababu ya kuleta mwalimu wa kigeni," alisema Kifaru.

Mtibwa Sugar wamemrejesha Omog nchini kwa lengo la kuziba nafasi iliyoachwa na Thieri Hitimana ambaye amejiunga na Simba.

# Michezo

Jumapili Septemba 19, 2021

Nipashe




Tuchel atabiri hatima ya Kane UKURASA 22



Mshambuliaji wa Azam FC, Iddi Nado (aliye juu), akijaribu kumtoka mchezaji wa Horseed ya Somalia katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam jana. Azam ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDANO**

## Alhaji Ndolanga afariki dunia Dar

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama Cha Soka Tanzania (FAT sasa TFF), Muhidini Ndolanga (71), alifariki dunia jana jijini Dar es Salaam.

Taarifa zilizopatikana kutoka kwa ndugu wa karibu zinasema Ndolanga alifariki jana mchana katika Hospitali ya TMJ, Dar es Salaam ambapo alikuwa akipatiwa matibabu.

Mara ya mwisho Ndolanga alishiriki katika mkutano mkuu wa TFF uliofanyika Agosti 7, mwaka huu jijini Tanga kama mgeni mwalikwa na alifungua mkutano huo kwa kuomba dua.

Ndolanga mmoja wa viongozi walioliongoza soka la Tanzania kwa muda mrefu, atakumbukwa kutokana na misimamo yake mikali na isiyoyumba kwa jambo alilokuwa alikiamini.

Aliiongoza FAT kuanzia mwaka 1992, akichukua nafasi ya Mohamed Musa na kudumu madarakani kwa miaka 12 hadi 2004.

Kiongozi huyo alishindwa kutetea nafasi yake baada ya aliyekuwa rais wa shirikisho hilo, Leodegar Tenga, kuingia kwenye awamu ya pili ya kupiga kura dhidi ya Katibu Mkuu wa zamani, Michael Wambura.

Ndolanga anashika nafasi ya pili kwa kuliongoza soka la Tanzania kwa muda mrefu, akizidiwa na marehemu, Said El Maamry ambaye naye alifariki dunia Julai, mwaka huu, aliyeongoza FAT kwa miaka 13. El Maamry alikaa madarakani kuanzia mwaka 1974 akirithi mikoba iliyoachwa na Ally Chambuso mwaka 1987.

Ndolanga alizaliwa Septemba 23, 1940 kwenye kijiji cha Nkunya Wilayani Newala na alianza elimu yake ya msingi kijijini Kitangiri, Newala na baadaye kujiunga na shule ya kati kuanzia darasa la tano hadi la nane kwenye kijiji cha Mahuta.

# Yanga yamaliza 'hesabu' Nigeria

## ●●● Wakati Simba Day ya kibabe leo huku Azam FC ikitakata CAF...

**Saada Akida na Tunu Hassan,** TUDARco

KIKOSI cha Yanga kinatarajia kuwakabili Rivers United katika mchezo wa marudiano wa hatua ya awali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Adokiye Amiesimaka jijini Port Harcourt, Nigeria kikiwa na ari na 'mzuka' wa hali ya juu.

**Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 na wenyeji wao, walipokutana katika mechi ya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.**

Msemaji wa Yanga, Haji Manara aliliambia gazeti hili walifika salama nchini Nigeria jana alfajiri na jioni walitarajia kufanya mazoezi ya mwisho kuelekea mchezo huo wa marudiano.

Manara alisema mechi zozote za mashindano ya Ligi ya Mabingwa zinazochezwa ugenini lazima ziwe ngumu na tunafahamu ugumu tutakaokutana nao tangu tutakapotua kwenye ardhi yao mpaka tutakapoondoka.

Alisema wachezaji, viongozi na mashabiki wote wa klabu hiyo walioko Nigeria wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wanaamini ushindi utapatikana na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Kesho (leo), kwenye Uwanja wa Adokiye, majira ya saa 10 alasiri, mabingwa wa kihistoria watafanya mazoezi ya mwisho kabla ya mechi ya Jumapili, tuko tayari kwa ajili ya mechi hiyo, wote tulioko hapa tuko tayari... nia yetu ni kwenda kuipigania klabu yetu, kwenda kuipigania nchi yetu," alisema Manara.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Benson Bana, aliwataka wachezaji wa Yanga wakapambane na kuhakikisha wanapata ushindi mnono katika mchezo huo.

"Nigeria ni salama, ubalozi ulijipanga, tunawaaomba mkapambane, msiwaangushe Watanzania," alisema balozi huyo.

**...LEO NI SIMBA DAY**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wanaikaribisha TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), katika mechi ya kirafiki ya Tamasha la Simba "Simba Day' itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Tamasha hilo ni maalum kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wa Simba watakaokitumikia kikosi chao katika msimu mpya wa 2021/22.

Simba kwa mara ya kwanza inaingia katika mchezo huo huku benchi la ufundi likiwa na makocha watatu Didier Gomes ambaye atasaidiwa na Thierry Hitimana na Seleman Matola.

Akizungumza jijini jana, Gomes, alisema anafuraha kubwa kukutana na Mazembe ambao ni wapinzani sahihi kwao katika maandalizi ya msimu mpya.

"Nataka kuwaonyesha mashabiki wetu kile tulichokuwa nacho, nawajua Mazembe tulikutana katika mashindano ya Simba Super Cup, walitupa changamoto nzuri, nina furaha kukutana nao tena," alisema Gomes.

Nahodha wa Simba, John Bocco alisema wamekuwa na maandalizi mazuri kuelekea msimu mpya na kukutana na TP Mazembe kwao ni kipimo bora.

Wakati huo huo Azam FC imesonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kupata ushindi wa jumla wa mabao 4-1 dhidi ya Horseed kutoka Somalia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >